

BARTIMAYO KIPOFU



Asante, Ndugu...?...

² Mwaweza kuketi. Hakika nina furaha kurudi tena, usiku wa leo. Nilikuwa tu nikizungumza na mke wangu hivi majuzi, nami nikamwambia, nikasema, “Ulipaswa kuwa huko, Mpenzi.” Hana budi kuwashughulikia watoto, bila shaka, nao wako shuleni, hao jamaa wadogo. Nami nikamwambia, nikasema, “Unapata kukutana na baadhi ya watu wazuri sana ulimwenguni papa hapa Texas, Louisiana, hawa watu wa kusini hapa.” Laiti ningaliweza kwenda nyumbani pamoja na kila mmoja wenu, nina hakika ningekula kiamshakinywa cha nafaka iliyokobolewa, uji wa nafaka iliyokobolewa, huo ni mzuri, hayo ndiyo maisha; mbaazi za macho meusi, na mboga za tanipu, ugali wa mahindi, hakuna kitu bora zaidi ni juuacho. Hicho ni kizuri.

³ Upendo wa Mungu hutufanyia mambo ya ajabu, sivyo? Jinsi unavyoishurutisha mioyo yetu, na kutuunganisha pamoja kuliko kitu kingine chochote kitakavyofanya, upendo wa Mungu!

⁴ Kesho usiku ni kufunga kwetu kwa kampeni hii, nami sina budi kukutana na wengi wa hao ndugu, na kuwaona, nami ninaninii tu, huu ni uamsho mmoja ambao hakika nachukia kuona ukimalizika, ni kwamba tu, wamekuwa wazuri sana, kila mtu ni mzuri sana.

⁵ Naye mama yangu alitoka Paris, Texas, nadhani mimi kidogo ni wa Texas. Kwa hiyo—kwa hiyo bila shaka nafikiri mna nchi nzuri sana. Na kinachoifanya nchi yoyote ni watu waliomo ndani yake, sawa. Louisiana, Georgia, na Alabama, na majimbo haya yote ya kusini, wanazungumza juu ya ukarimu wa kikusini, hiyo ni kweli.

⁶ Na usiku wa leo tunapanga sasa... Nilimwomba Ndugu Moore azungumze kidogo kwa niaba yangu, na Don, kusudi isinibidi kuhubiri. Na ninii tu, jana usiku tulikuwa na mchezo mdogo wa kuigiza, hadithi ndogo, labda tungeweza kuwa na nyingine ya hizo fupi usiku wa leo, kabla tu sijawaombea wagonjwa.

⁷ Halafu kesho usiku, natumaini, labda, kama ingekuwa ni mapenzi ya Bwana, ningetaka kuzungumza nanyi tena, labda juu ya somo, mahubiri kwenye ibada ya kumalizia. Hakika tunathamini yote ambayo mmefanya, mmekuwa wazuri sana, kweli, wazuri sana.

⁸ Nami nina furaha kwamba upendo wa Mungu unatufanya tufikie, mbali sana. Tunaweza kuona mambo ambayo hatujawahi kuona hapo kabla. Na wakati mwingine mikutano kama hii ina ushawishi maalum juu ya watu kuwashawishi ku—

ku—kupata ono la kile Mungu anachomaanisha, nafikiri ina—inawasaidia watu.

⁹ Sasa, usiku wa leo mimi, kabla hatujafungua Maandiko, ninataka kusema ya kwamba ninataka kungoja mpaka nitakapoanza kuwaombea wagonjwa kabla sijaomba juu ya maskini leso hizi, na nguo, na kadhalika, ama chochote kile. Na sasa, kama ukikosa kuweka moja hapa, laiti ungeagizia, upate moja, kwa vyovyote vile. Ni bure, hatuuzi chochote. Hata vitabu vyetu, mtu mwingine huvichapisha, na karibu vyote tunanunua kwa punguzo la asilimia arobaini, ili tuweze kuvileta. Nawe huninii. . .

¹⁰ Bila shaka hawapati faida yoyote kwenye vitabu hivyo, kwa sababu ya hasara tunayopata kwake, na uharibifu. Nami daima nimewaambia hao wavulana, kama mtu fulani akija na hawakuwa na pesa za kukinunua na anakitaka, wapeni. Mnaona? Acha tu wakichukue, kwa vyovyote vile. Lakini vitabu hivyo vimechapishwa, kimoja na Julius Stadskev, viwili ama vitatu, na Ndugu Lindsay, na kadhalika. Nasi tunavinunua kwa, nafikiri, punguzo la asilimia arobaini, nafikiri hivyo ndivyo ilivyo, na hata hivyo, hao wavulana hushughulikia hilo.

¹¹ Hatuna mpango wa pesa, pesa hazihusiki hata kidogo. Mhudumu mmoja alinipigia simu hivi majuzi, na kusema, “Sasa, mpango wako wa kifedha ukoje? Tunapaswa kuwa na pesa ngapi?”

Nikasema, “Hakuna.”

Naye akasema, “Vema, unapataje riziki?”

¹² Nikasema, “Vema, kwa kawaida mwishoni mwa ibada wanatoa sadaka ya upendo,” nikasema, “kama wao, watu wakijisikia kufanya hivyo; wasipojisikia, mbona, hilo ni sawa kabisa, pia.” Na kama—kama hawalipii matumizi, wanaweka hizo kwenye matumizi, na kutuacha tuyalipie. Wasipofaulu, basi tutaagizia nyumbani na kuliacha kanisa langu liyasimamie. Tunataka daima kubeba jina hilo la kutoninii kamwe. . .

¹³ Nisingemruhusu mmoja wa watu wangu, kamwe, kamwe, kuombaomba ama kuwa mdoezi wa pesa. Inapofikia mahali hapo, ni wakati wangu wa kutoka hudumani basi. Mnaona? Naam. Kama Mungu hatoi kwa ukarimu kila kitu tunachohitaji, ni wakati wa kuondoka. Nafikiri mikutano mingi inaharibiwa na yote hayo ati “Ni nani atakayetoa kumi? Ni nani atakayetoa tano?” Sipendi hilo. Kuna jambo moja tu ambalo ninapenda kusikia habari zake, kwamba—kwamba. . .

¹⁴ Je, nilisema jambo baya? Na—natumaini sikusema lolote baya, nilikuwa tu nikiuelezea moyo wangu, jinsi tu nilivyojisikia. Lakini ninaamini kuna kitu kimoja tu ninachotaka utoe, utoe moyo wako kwa Kristo, hicho tu ndicho ninachohitaji, mpe tu Kristo moyo wako, hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa. Na

kwa hiyo nina hakika ya kwamba Mungu atayashughulikia hayo mengine, kama tu utafanya hivyo.

¹⁵ Na sasa, kabla hatujalikaribia Neno usiku wa leo, na tuombe, tunapoinamisha vichwa vyetu. Ni nani angetaka kukumbukwa katika maombi usiku wa leo tu? Akisema, “Nikumbuke, Bwana, mimi—mimi ni mhitaji. Ikumbuke haja yangu, Bwana.”

¹⁶ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja tukikaribia kiti Chako cha rehema. Tusingekuja tukikaribia haki, kwa sababu tusingeweza kuistahimili, tusingeweza kuikaribia sheria Yako, kwa sababu haina ukombozi, bali tunamkaribia Yesu, Ambaye ni rehema Yako, nasi tunakuja tukiomba rehema ya Kiungu juu yetu sote.

¹⁷ Tusamehe upungufu wetu, na makosa yetu, na mambo ambayo tumefanya, ama kusema, ama hata kuwazia ambayo yalikuwa ni mabaya.

¹⁸ Nasi hatuamini ya kwamba sisi ni watakatifu, Bwana, tunaamini si mlima mtakatifu, bali ni Mungu Mtakatifu juu ya mlima, si kanisa takatifu, bali Roho Mtakatifu ndani ya kanisa, si watu watakatifu, Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, Baba, tunaomba sasa, kwamba Roho Mtakatifu atatushughulikia kwa huruma usiku wa leo tunapowashughulikia wagonjwa na wanaoteseka. Bwana, wao ni dhaifu, na ni wagonjwa, na ni wahitaji.

¹⁹ Nasi hatujui jinsi ya, jambo la kufanya, Bwana, ninasimama hapa katikati ya maoni mawili wakati huu, jinsi tu ya kuliendea somo dogo hapa, nikishangaa kama Wewe ungelibariki kwa mioyo ya watu. Jalia niweze kusema jambo ambalo lingehimiza imani, ambalo lingechochea karama iliyo ndani ya watu, wapate kupokea uponyaji wao usiku wa leo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁰ Zaidi ya mambo yote, Bwana, mtu huyo mwenye ugonjwa wa dhambi aliyeketi hapa, popote alipo, ninaomba, Mungu, ya kwamba wataona Nuru ya mchana ikiangaza, nao watakuja na kupatanishwa kwa Damu iliyomwagika ya Bwana Yesu. Tujalie.

²¹ Ninaliombea kundi hili zuri la watumishi Wako walionunuliwa Kalvari hapa nyuma yangu, Bwana. Ninajisikia duni sana kusimama hapa jukwaani mbele ya watu hao, na baadhi yao walikuwa wakihubiri Injili nilipokuwa tu mvulana mwenye dhambi. Mungu, ninaomba ya kwamba utaibariki hiyo mioyo yenye ushujaa. Jalia washikamane pamoja, Bwana, kwa kuzungushiwa upendo wa Mungu hivi kwamba, Baba, kwamba wata—watafanikiwa katika lolote wafanyalo. Jalia wawe watumishi hodari kumleta Kristo kwa watu katika saa hii ya kumalizia historia ya ulimwengu.

²² Waponye wagonjwa wote na wanaoteseka, nafsi na mwili pia, Baba, tunaomba. Tubariki pamoja, tunapolingojea Neno Lako sasa, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

23 Katika Kitabu cha Injili ya Luka Mtakatifu, mlango wa 18 na kifungu cha 38:

Akapiga kelele, . . . Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu.

24 Na katika kifungu cha 42:

. . . Yesu akasema . . . Upewe kuona, imani yako imekuokoa.

25 Hadithi yetu ndogo inaanza usiku wa leo, na ilikuwa kwenye asubuhi yenye baridi, ya majira ya kuchipua upande wa mashariki tu wa lango la Yeriko ambapo barabara inashuka kutoka Yerusalemu. Ulikuwa usiku mbaya kwa maskini jamaa huyo, hakuweza kulala hata kidogo, aligaagaa tu, angeamka, na kugaagaa. Usiku huo wa kutisha, tunajua ni nini, karibu sisi sote. Alisumbuliwa na wasiwasi, na ilionekana kana kwamba ulikuwa ni usiku mbaya sana.

26 Yeye, na wakati alipoamka, naye alikuwa amechelewa kufika kwenye kituo chake, ambapo alifanyia kazi yake ya kila siku kwa kuombaomba. Kulikuwa na ombaomba wengi mjini na kote nchini siku hizo, nchi maskini sana, na watu maskini chini ya utumwa wa Milki ya Kirumi. Iliwabidi ombaomba kufika mtaani mapema sana, na kila mmoja alikuwa na mahali alipokaa, alipotengewa. Nao wangesimama hapo, ndipo wakati wafanyabiashara wangeshuka mtaani, wangelia wapewe sadaka.

27 Naye mfanyabiashara, labda, ombaomba wa kwanza aliyekutana naye na kumpa kipande cha fedha, mbona, hiyo labda ilitosha kwa siku hiyo, kwa sababu asingemudu kutoa nyingi kupita kiasi, kwa sababu labda asingeweza kumudu kila siku kutoa sarafu, dinari ya Kirumi, ama chochote kile, huenda ilikuwa ni nyingi sana kwake. Kwa hiyo, aliweka ndani sarafu yake, halafu akatoka. Na labda jamaa huyo mwingine akapata sarafu kutoka kwa mtu mwingine.

28 Lakini iliwabidi wawe huko mapema wakati wafanyabiashara walipoingia katika maeneo yao, biashara, na masoko. Kulikuwako na sehemu nyingi ombaomba wasingeweza kusimama, kwa hiyo wangeweza, askari wangepatenga mahali, nao iliwabidi kusimama hapo.

29 Basi rafiki yetu usiku wa leo tunayemjua kama Bartimayo, baadhi yao wanalitamka *Bartimayo*, mbona, tunamwona amechelewa kwenye kituo chake. Na mahali pake palikuwa tu upande wa kaskazini mwa lango, ambapo alisimama langoni kuwashika wafanyabiashara walipoingia, na ilionekana kana kwamba alikuwa na mahali pazuri sana. Naye alikuwa kipofu tangu alipokuwa jamaa mdogo.

30 Basi usiku huo . . . Sababu ya kuchelewa asubuhi hiyo, tutasema, na, kulifanya mchezo wa kuigiza, kwamba alikuwa

ameota usiku kucha kwamba angeweza kuona tena, alikuwa amewazia ya kwamba angeweza kuona tena anga, na nyota, na nuru ya jua. Lakini sasa, aliishi katika ulimwengu wake peke yake, amefungiwa gizani kabisa, kipofu.

³¹ Nafikiri moja ya mambo ya kutisha sana ni mtu kipofu. Nami ninasikitika ninapomwona mwanamume ama mwanamke mtaani akiwa na hiyo fimbo nyeupe, akitembea akipigapiga. Mara nyingi nimesimamisha gari langu, na kumkimbilia, na kumwona maskini mama fulani akiwa karibu kugonga kizingiti, ama chochote kile, huko chini mtaani, na kumsaidia kuvuka, jamaa mdogo, ama mzee. Upofu, nafikiri ndilo jambo la kusikitisha sana.

³² Lakini mimi... Kuna—kuna upofu ambao ni mbaya kuliko upofu wa kimwili, huo ni upofu wa kiroho. Ninawahurumia zaidi kuliko ninavyowahurumia vipofu wa kimwili. Kwa hiyo kwa nini mioyo yetu isiwaendee, badala ya kuwahukumu? Hebu na tuwapende, ndipo wataona Nuru, kama tu utawapenda. Ulimwengu unakufa, si kwa ajili ya uchumi bora; kanisa linakufa, si kwa ajili ya majengo bora, dhehebu kubwa zaidi, bali linakufa lipate mtu wa kulinyoshea mkono wa upendo, kuonyesha ya kwamba tunajaliana sisi kwa sisi. Na hiyo ndiyo ishara yenyewe ambayo Yesu alitwambia kwamba, “Kwa hii watu wote wangejua ya kuwa ninyi mlikuwa wanafunzi Wangu,” wakati tukipendana.

³³ Nilikuwa nikiwazia juu ya kipofu, kidogo iko nje ya somo langu, lakini pia si nje, kulikuwa na kipofu Fanny Crosby, angeweza kuona vizuri kuliko watu wengi walio na macho mawili mazuri. Walijaribu kumfanya, wakati mmoja, aandike muziki ama mashairi ya ulimwengu wa dansi, na kwa ulimwengu wa burudani, naye akakataa kufanya hivyo, kwa hiyo walikuwa wakimdhihaki.

³⁴ Nikawazia, “Ni tofauti jinsi gani kati yake, na maskini mvulana fulani, wa Kipentekoste, ambaye ameuwasha moto ulimwengu kwa roki!” Mara nyingi nimewazia kwamba yeye ni mbaya kuliko Yudasi. Yudasi, Esau aliua haki zake za mzaliwa wa kwanza. Na ni jambo la kuchukiza jinsi gani ambalo kijana mwanamume huyo atapaswa kuwajibika kwenye Siku ya Hukumu, aliwapeleka watu wengi kuzimuni kuliko vilabu vyote vya pombe haramu vilivyoko nchini. Hiyo ni kweli.

³⁵ Halafu basi, wakati Fanny Crosby, siku moja walipomjia na mapatano haya makubwa, alikuwa maskini, pia, nao wakamjia, na kusema, “Tutatoa *kiasi fulani*, kama tu ukichangia kipaji chako katika kutunga nyimbo za ulimwengu wa burudani,” akakataa katakata, asingefanya hivyo.

Akasema, “Kama kuna chochote nilicho nacho, ni cha Kristo.”

36 Na kwa hiyo wao, wale wanaume waliokuwa wakizungumza naye, wakasema, “Basi nadhani ya kwamba unatarajia kwenda kwenye Ulimwengu ambamo kuna Uzima wa milele, na kadhalika?”

Kasema, “Naam.”

“Kwa hiyo unamtarajia huyu Kristo awe nini?”

Kasema, “Yeye atakuwa ni Mwanamume.”

Kisha kasema, “Basi kama wewe uko vilevile ulivyo hapa,” kasema, “kamwe usingemwona,” kasema, “wewe ni kipofu.”

Akasema, “Loo, nitamjua, kwa vyovyote vile.”

37 Kwa hiyo wakasema, “Ungewezaje kumjua, kama ungali kipofu kule, kwa kuwa hujawahi kuona katika maisha haya? Na upande ule mwingine, kama huna macho kule, ungemjua je basi?”

Akasema, “Nitamjua.”

38 Nao wakamcheka, naye akageuka na kuanza kutembea kote kwenye nyumba. Alipokwisha kufanya uamuzi wake, “La, bwana, hakuna kitu cha ulimwengu! Kipaji changu chote amepewa Kristo.” Nao wakasema . . . Akaanza kurudi nyumbani na kuinua mkono wake, akasema:

Nitamjua, nitamjua,
Na huku nimekombolewa karibu Naye
nitasimama;
Nitamjua, nitamjua,
Kwa alama za misumari mkononi Mwake.

39 Ni kwenye nyakati hizo kuu, za hatari ambapo ma—majaribu yamewekwa juu yetu ambapo Mungu huingia, tunapofanya uamuzi kwa ajili Yake. Hiyo ni kati ya Uzima na mauti, ncha hiyo ndogo yenye makali. Wakati mwingine wakati wa mwisho unapofikiri hutapona, na mtu fulani anakudhihaki, huku ungali umeshikilia ushuhuda wako, ni wakati huo ndio Mungu huingia.

40 Bartimayo alikuwa amewasili jukwaani kidogo amechelewa. Kwa hiyo, ilikuwa msimu wa kuchipua asubuhi na mapema, naamini, mnamo Aprili, maana ilikuwa karibu na Pasaka. Na nguo zake zilikuwa zimechakaa kabisa, nadhani. Ndipo akafika langoni, kulikuwa kimya, kwa hiyo akasema, “Vema, nimechelewa kidogo kwa sababu nililala kupita kiasi.” Lakini jua katika anga za Palestina lilikuwa tu, labda, likichomoza mashariki, naye kwa namna fulani upande wa kaskazini akatupa ninii. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . juu ya ukuta, mahali ambapo uliporomoshwa na kuangushwa na Mungu, wakati Yohana alipoingia.

41 Hebu na tuwazie alijitafutia jiwe, akaketi kwenye mwanga wa jua, kasema, “Vema, labda kuna mfanyabiashara mmoja

amechelewa kidogo. Nitapata sarafu, labda, leo kwa ajili ya familia yangu, maana kweli tuna mahitaji.”

⁴² Ndipo akaanza kuwazia kuhusu, wakati alipokuwa ameketi pale kwenye mwanga wa jua wenye joto, amejifunika koti lake lililochakaa, akaanza kuwazia juu ya ndoto yake, jinsi ilivyokuwa halisi. Ndipo akili yake ikaelea tena katika ndoto ya mchana, kama vile ninavyojua sote tuna matukio hayo.

⁴³ Mara nyingi, ningeweza kupanda juu sana mlimani hata nikawa umbali nisioweza kusikia kutoka kwa chochote, kitu chochote, nimeketi tu pale pamoja na wa—wanyama, na kuota, loo, kuota tu juu ya Mungu, na Kuja kwa Bwana, na kuangalia huko nje na kumsikia akipiga makelele katika ndege, na kumwalia katika tai, na kumwona katika kuchomoza kwa jua na kutua kwa jua; Yeye amekuzunguka tu kote. Kuwa peke yako na uote ndoto.

⁴⁴ Kwa hiyo Bartimayo, labda, alikuwa ameketi huko nje katika ndoto, namna hiyo. Na kwa kuwa ilikuwa ni majira ya kuchipua, alisema, “Loo, niliota jana usiku kwamba nilikuwa ninaona! Ninaweza kukumbuka nilipokuwa mvulana mdogo, tuliishi karibu tu na mlima hapa, kibanda kidogo karibu pembeni pale, ninii yangu... Nakumbuka nilipokuwa mapema katika majira haya ya kuchipua, wakati makombe-mtindi madogo yangechipuka, jinsi nilivyokuwa nikikimbia nje kama mvulana mdogo na kucheza, naye Mama angeniruhusu kumchumia shada dogo la maua.

⁴⁵ “Na jinsi ningeonekana, nimelala huko nje kwenye vitanda laini vya nyasi, niangalie juu na kuona mawingu meupe yakipita katika Aprili, mwanga wa jua wenye joto ukiniwakia. Jinsi hapana shaka ulimwengu huu ulivyo mzuri! Ila sijauona kwa muda mrefu, kwa miaka mingi ya upofu, kwa hiyo nadhani kamwe sitaona. Lakini loo, jinsi ninavyoithamini ndoto hiyo jana usiku, hata kuota kwamba ningeweza kuona!”

Ndipo akaanza kuwazia, akili yake ikashikwa, loo, huo ni wakati unapoingia katika roho ya chochote kile, akarudishwa huko nyuma alipokuwa mvulana mdogo.

⁴⁶ Ninajua sisi sote hufanya hivyo. Mimi hufanya hivyo, ninarudi kwenye wakati nilipokuwa mvulana mdogo, namwona baba yangu akiingia pamoja na, jamaa mdogo, mfupi, mkata miti, na jinsi alivyokuwa na mikono yenye nguvu, nami ningemwona... Hakuwa na uzito wa yapata ratili mia moja na arobaini, lakini jamaa fulani aliniambia hivi majuzi alimwona akipakia gogo la ratili mia tisa na hamsini peke yake kwenye mkokoteni.

⁴⁷ Nami ningemwona, wakati angekunja mikono ya nguo yake, mtofaa wa kale pale, na kipande kidogo cha kioo alichokibandika mama juu yake, na bomba dogo la gudulia. Alikuwa na gunia la unga kwa ajili ya taulo, ningemwona

Baba akivuta maji kwa bomba na—na kuchukua sabuni na kunawa mikono yake, sabuni hiyo ya kale ya magadi tuliyokuwa tukitengeneza, mwajua, na kutengeneza magadi, na kutengeneza sabuni kwayo, na kuoga. Nilipomwona akinyosha mikono yake juu namna *hiyo*, kuchana nywele zake nyeusi zenye matimutimu, nikasema, “Wajua, baba yangu hatakufa kamwe, ana nguvu sana hawezi kufa.” Lakini alikufa akiwa na umri wa miaka hamsini na miwili.

⁴⁸ Ndipo ninawazia juu ya Waebrania 13, “Hapa hatuna mji udumuo, bali tunautafuta ule ujao.” Hatuna mahali pa kudumu hapa, sisi ni wasafiri, nasi ni wageni hapa, tunautafuta Mji ujao.

⁴⁹ Sasa, Bartimayo akikumbuka alipokuwa mvulana mdogo, nami naweza kuwazia alikuwa akiwazia hili: “Loo, ninakumbuka kwenye wakati wa chakula cha mchana, ningesikia hiyo sauti tamu ya yule mama yangu mrembo ubavuni mwa kilima, ‘Bartimayo, karibu chakula chako cha kutwa, Mwanangu!’ Na jinsi ningekimbia nyumbani, naye angeuosha maskini uso wangu, na kuzirudisha nyuma nywele zangu, na kunibusu mashavuni, nami ningeona macho yake makubwa, laini, nami nikauangalia uso wa mama huyo mrembo, na—naye angeniketisha kwenye chakula cha mchana.

⁵⁰ “Halafu, baada ya chakula cha mchana, katika muda kidogo angeniita tena, maana ilikuwa ni wakati wa kulala kidogo. Naye angeketi nje barazani huku tumeiangalia Yordani, naye angenipembeza mikononi mwake, nami ningeweka mikono yangu ya kitoto kwenye mashavu yake mazuri, naye angenibusu, na—naye angenisimulia hadithi za Biblia. Na jinsi nilivyopenda kusikia hadithi hizo, jinsi Yehova Mungu mkuu alivyowaleta watu wetu katika nchi hii ya ahadi!

⁵¹ “Naye angeangalia kwenye yale makombe-mtindi madogo ambayo nilimletea, yale maua madogo kutoka ubavuni mwa kilima, naye angesema, ‘Hayo ni baadhi ya ahadi ya Yehova pia, Bartimayo. Nchi hii nzuri ni yetu, naye Yehova alituingoza kutoka vichungu vikubwa vya mchanga vya Misri, na kutuweka katika nchi hii.’

⁵² “Jinsi angeniambia juu ya yule Yehova mkuu, mwenye nguvu, jinsi alivyonguruma kwa ajili ya watu Wake, akasimama kwenye pengo, akalizamisha jeshi la Farao lililokuwa nyuma yake, jinsi alivyoshusha chakula kutoka Mbinguni, akaleta kware kutoka kondeni, akawalisha watu wetu, na jinsi alivyofanya ishara, maajabu. Walipokuwa na kiu, yule nabii mkuu Musa aliupiga Mwamba, na maji yakatoka.

⁵³ “Loo, jinsi Yehova alivyokuwa mkuu! Ni Mungu mkuu, mwenye nguvu jinsi gani tunayemtumikia! Jinsi ambavyo Yehova mkuu alikuwa amemwahidi yule nabii Musa, ‘Siku moja Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo

mimi,' Naye atatuondoa chini ya utawala huu wa kimabavu wa Kirumi.”

⁵⁴ Halafu basi, mnakumbuka wakati walipovuka Yordani, kidogo tu chini ya mahali kibanda chao kilipokuwa, na jinsi ambavyo Yehova aliifingirisha nyuma bahari, Yordani, katika mwezi wa Aprili wakati vilima vya theluji vilipokuwa vikiyeyuka katika Uyahudi, juu karibu na mlima, Hermoni, na kadhalika? Na maji haya ya barafu, ya theluji yalikuwa yakibubujika, na yamejaa matope, yakifingirika, yule Yoshua mkuu, mwenye nguvu alishuka akaenda baharini na kunena, naye Yehova akarudi kwenye nchi kavu kama unga, na kuwavusha, moja kwa moja katika mwezi wa Aprili. Loo, jinsi ambavyo Mungu huyo mkuu. . .

⁵⁵ Ndipo Bartimayo akaangalia huko kidogo, kidogo akatetemeka, na kusema, “Mnajua, laiti Yehova angalikuwa bado ni Yehova, kwa namna fulani, ninaamini ndivyo alivyo, ila kuhani wangu ananiambia ya kwamba mambo hayo yote yamepita, Yeye si kama. . .”

⁵⁶ Mara anasikia kitu fulani kikija, *kacha, kacha, kacha, kacha*, ni maskini punda mmoja. Vema, huyo hapana shaka ni tajiri, kwa sababu usafiri wakati huo kwa kawaida ni kwa, maskini walitembea kwa miguu, matajiri walienda kwa mkokoteni uliokokotwa na punda, ama walipanda mgongoni mwa punda. Kwa hiyo anasimama, anaenda haraka kama futi ishirini kwenye barabara kubwa ya mango, na kukimbia nje, na kusema, “Sadaka kwa kipofu! Sadaka kwa kipofu!”

⁵⁷ Mara ghafla maskini huyo punda akasimama, naye akasikia sauti ya kikatili ikisema, “Simile nipite, ombaomba! Mimi ni mtumishi wa Bwana. Niko njiani kwenda Yeriko asubuhi ya leo, ninaenda kukutana na shirika la wahudumu, nami nitahakikisha ya kwamba hakuna ibada za uponyaji hapa, hakuna chochote cha huo ulokole. Hakuna mtu yeyote *anayejiita* nabii wa Galilaya atakayekuja hapa na ulokole wake wowote. Simile nipite, ombaomba, sina budi kuendelea na safari, niko kwenye huduma ya Bwana.”

“Samahani, ewe mtakatifu.” Akarudi nyuma.

Moja kwa moja anaelekea Yeriko, kuhudhuria ninii. . . kulifanya shirika la wahudumu likomeshe miamsho yote kama hiyo.

⁵⁸ Labda hilo kidogo ni fidhuli, labda sikupaswa kusema hivyo. Jambo lingine, mwajua, mtu hufa, bali roho hafi, kwa hiyo ni baya sana, lakini hilo, hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa, kwa maana kila kizazi kitakachosimama kwenye Hukumu kitapaswa kukabiliwa na jambo lile lile, mnaona, huna budi kupitia jambo lile lile, hasa, jambo.

⁵⁹ Ndipo wakati Bartimayo alipokuwa akirudi, ilikuwa inaingia mchana, hebu tuwazie, kidogo, nalo jua sasa lililokuwa

likipita lilikuwa limelifunika lile jiwe kwa kivuli, kwa hiyo akapapasa-papasa kote mpaka akapata lingine, akaketi chini. Akawazia, “Vema, nadhani sitapata chochote usiku wa leo, nadhani itatubidi tu kuondoka mikono mitupu.”

⁶⁰ Basi alipoketi chini, akawazia, “Vema, nilikuwa na ndoto nzuri sana kuhusu siku zilizopita, na kuhusu Yehova mkuu.” Ndipo akachukua wazo lake tena, na kusema, “Naam, ninakumbuka Mama akinisimulia moja ya hadithi ninazozipenda sana; na moja ya hadithi nilizozipenda sana ilikuwa ni hii, alizoea kuniambia juu ya nabii Eliya. Ninaipenda hiyo vizuri sana, kwa sababu angesema ‘Bartimayo, je, unaienda hadithi ya Eliya Mtishbi na yule mwanamke Mshunami?’

⁶¹ “Naam, Mama, kwa sababu inahusu mvulana mdogo, na jinsi Mungu alivyotekeleza mpango wake kwa mvulana mdogo.” Naye aliipenda hiyo, kwa sababu alimwamini Yehova, pia.

⁶² “Naye mwanamke huyu Mshunami, akiwa ni Mmataifa, hata hivyo Mungu alimpa fadhili. Jinsi yule nabii mkuu Eliya, mwenye nguvu, alivyokuja humo mjini, naye akatambua ya kwamba alikuwa ni mtu mtakatifu. Naye aliishi katika pango huko juu mlimani, na alikuwa pamoja na mtumishi wake, Gehazi,” ambaye kwa namna fulani alikuwa kama meneja wa uamsho aliyeenda kote, na kumsaidia kutayarisha mambo wakati angezungumza. “Na *kwa namna fulani* alimpenda mtu huyu, alifikiri alikuwa ni mtu mzuri sana.

⁶³ “Kwa hiyo mumewe alikuwa kidogo ni mzee, naye alikuwa anazeeka. Akamwambia mumewe, ‘Nakusihi, na tumfadhili mtu huyu, kwa maana naona ya kuwa ni mtu mtakatifu.’

⁶⁴ “Basi wakajenga chumba kidogo kando ya nyumba yao, chumba kidogo, cha nabii, wakamwekea kitanda kidogo mle na—na, pia, wakamwekea jagi ndogo ya maji, na kiti kidogo cha kukalia, na karai ndogo ya kuoshea miguu yake iliyochoka, na viungo vilivyochoka wakati akiketi chini. Na hapana shaka huyo mtumishi angemletea chakula alipomsikia huko nje chumbani.

⁶⁵ “Naye Eliya akapendezwa sana na jambo hili, hata,” ninaweza kumsikia akisema, “Bartimayo, unajua kile mwanamke huyo alichohitaji sana kuliko vyote alipouliza? Akasema, ‘Nikupe fadhili gani? Ninaweza kukuomba neno kwa mfalme, au nikutendee nini?’

⁶⁶ “Akasema, ‘La, ninakaa pamoja na watu wangu mwenyewe, sihitaji chochote. Nilifanya hivyo tu kutoka, moyoni mwangu kwa sababu ninamheshimu Mungu unayemtumikia, pia nayaheshimu maisha unayoishi.’

“Ndipo Gehazi akasema, ‘Yeye ni mkongwe, mumewe ni mzee, wala hawana watoto.’” Bartimayo aliipenda hii.

⁶⁷ “Ndipo yule nabii mkuu Eliya akasema, ‘Nenda, mwambie asimame hapa mlangoni.’” Alikuwa ameona ono. “Akasema, ‘BWANA ASEMA HIVI: Utamkumbatia mwana.’

⁶⁸ “Ndipo mvulana huyu mdogo alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili, loo, jinsi baba na mama yake walivyompenda!” Huo hapana shaka ulikuwa ni yapata umri wa maskini Bartimayo. “Na jinsi ambavyo baba na mama walimpenda! Jinsi ambavyo baba alimpeleka huko nje kondeni, na kumwonyesha mbinu zote za kulima nafaka. Siku moja alipokuwa huko nje kondeni, hapana shaka aliathiriwa na jua kali, kwa sababu aliendelea kusema, ‘Kichwa changu, kichwa changu!’” Hilo jua la Palestina ni kali, ile miale yake ya moja kwa moja. “Kichwa changu, kichwa changu!

“Naye, baba alikuwa na shughuli nyingi, kwa hiyo, huyo mvulana alikuwa ni mgonjwa, akamwambia mtumishi, ‘Mpeleke huyu mtoto kwa mama yake.’

⁶⁹ “Basi huyo mvulana akazidi kuwa mgonjwa, mpaka hatimaye, pajani mwa mama yake, akafa. Ndipo ushujaa wa mwanamke huyo maarufu, aliyemfadhili mtumishi wa Kristo, alijua kabisa, na aliongozwa na Roho jambo la kufanya.” Loo, napenda hilo! Si Bartimayo tu, bali napenda hilo. “Akampeleka kwenye chumba cha nabii na kumlaza juu ya kitanda cha nabii.” Ni mahali pa jinsi gani pa kumlaza! Sawa kabisa.

“Ndipo akamwambia mtumishi wake, ‘Nitandikie nyumbu, wala usisimame hata nitakapokwambia. Twendelee mbele.’

Ndipo mumewe akasema, ‘Hakuna haja ya kumtafuta, huu sio mwandamo wa mwezi wala sabato, yeye hayuko huko juu.’

“Akasema, ‘Yote ni sawa.’

⁷⁰ “Na jambo lingine, Bartimayo, unajua Mungu hawafunulii watumishi Wake kila kitu? Yeye huwafunulia tu yale anayotaka wajue,” unaona, “yale tu anayotaka wajue. Kwa hiyo huyo mwanamke alipomkaribia mtu huyu mkuu, mwenye nguvu wa Mungu alienda mlangoni mwa pango lake, na kuweka fimbo yake kando ya ukuta, kidogo anazeeka, naye akainua mikono yake *hivi*, kisha akaangalia nje, akasema, ‘Ni nani yule ninayemwona akija?’

“Gehazi akasema, ‘Ni yule Mshunami. Anaonekana kana kwamba amejaa huzuni.’ Alikuwa akilia na kwenda mbele.

“Kwa hiyo akasema, ‘Moyo wake una huzuni, lakini Mungu amenificha, sijui ana shida gani.’ Kasema, ‘Nenda, ukamlaki.’

⁷¹ “Naye akaenda akamlaki. Ndipo alipomkaribia nabii huyu mkuu, akasema, ‘Hujambo? Mume wako hajambo? Mwanao hajambo?’”

⁷² Loo, napenda usemi wa mwanamke huyo! “Alisema, ‘Hatujambo.’”

⁷³ Nafikiri hapo ndipo Martha na Mariamu, Martha sikuzote alikuwa mzembe, ilionekana hivyo, lakini alipojua kwamba iwapo, akimrejelea mwanamke huyu, iwapo mwanamke huyu Mshunami alijua ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya nabii huyo, huyo alikuwa ni mwakilishi wa Mungu wa siku hizo, na kama Mungu alikuwa ndani ya nabii Wake, ni zaidi sana vipi alivyokuwa ndani ya Mwanawe!

⁷⁴ Naye akasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa ndugu yangu asingalikufa, lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupaa.” Jambo ndilo hilo. Wazo ndilo hilo.

⁷⁵ Naye yule mwanamke Mshunami, akasema, “Hatujambo.” Kwa nini? Mumewe anakunja mikono yake na kupiga mayowe, jamaa wote wanapiga mayowe na kuomboleza, na kupiga makelele, naye huyu hapa amehuzunika sana, mtoto mchanga amelala kwenye kitanda cha nabii, amekufa, mwanawe wa pekee, naye ni mwanamke mkongwe, mwanamume mkongwe. Jinsi alivyompenda maskini jamaa huyo! Lakini, “Hatujambo,” kwa kuwa alikuwa amesimama mbele ya mwakilishi wa Mungu.

⁷⁶ Naye alijua . . . alijua ya kwamba Mungu angeweza kufunua kupitia kwa mwakilishi huyo chochote kilichokuwa. “Mungu alitoa, na Mungu ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe.” Lakini alitaka kujua ni kwa nini Mungu alimchukua. Ninapenda hilo.

⁷⁷ Naye Mungu ana Mwakilishi ulimwenguni siku hizi, tunamwita Roho Mtakatifu, simama Uweponi Mwake. Ee Mungu, laiti watu wangeweza kupata hilo. Simama Uweponi Mwake uone kile Yeye asemacho.

⁷⁸ “Naye akasema, ‘Hatujambo.’ Nadhani moyo wa nabii ulichangamka. Kwa hiyo, akaja, akaanguka chini, na kumshika miguuni. Huo ulikuwa kwa namna fulani utovu wa uadilifu, aliwazia mtumishi, mwanamke huyu hapaswi kumwangukia bwana wake namna hiyo, kwa hiyo alifanya nini, ila kumnyanyua.

⁷⁹ “Na kwa hiyo Eliya akasema, ‘Mwache, moyo wake umejaa huzuni, na Mungu amenificha.’

⁸⁰ “Ndipo basi akafunua yaliyokuwa yametukia, kasema, ‘Kwa nini Mungu akanipa huyu mwana? Kwa nini uliniambia hivyo ili kunidanganya? Sasa mvulana huyo amelala amekufa.’

⁸¹ “Mwangelieni Eliya, alisema, alijua ya kwamba kila kitu alichogusa kilibarikiwa wakati alipotiwa mafuta, akamwambia Gehazi, ‘Chukua fimbo hii kisha utangulie, na mtu akikusalimu, usimsalimu. Usisimame kwa mambo yoyote ya kijamii.’”

⁸² Nafikiri hivyo ndivyo Mungu afanyavyo kwa Neno Lake, Hilo limetiwa Mafuta, ni Yeye, nasi ni wajumbe Wake. Hatuna wakati wa kusimama kufanya jambo *hili*, na kubishania *hili*, na kuzozania *hili*, Ujumbe ni wa dharura, watu wanakufa, hebu tufike kule, tukomeshe vizuizi vyetu vya kimadhehebu, na kila

kitu kingine, na tupenye. Naam, bwana. Tuupeleke Ujumbe kwa ulimwengu unaokufa. Halafu. . . Sitaki kuingilia hilo, nitaanza kuhubiri.

⁸³ “Sasa, hata hivyo, akaanza kwenda mbele. Bali imani ya huyo mwanamke haikuwa katika ile fimbo, imani yake ilikuwa katika huyo nabii, naye akasema, ‘Kama Bwana Mungu aishivyo, nafsi yako haifi,’ alijua alikuwa hai milele, ‘nafsi yako haifi kamwe, sitakuacha.’” Loo, jamani! Jambo ndilo hilo, sasa umelipata, endelea kushikilia. Mshikilie Roho Mtakatifu namna hiyo wala usimwachilie. “Mkono wangu ni bora zaidi leo, haileti tofauti yoyote kesho, haileti tofauti yoyote, wakati wowote ule, nitashikilia, kwake itakuwa sawa. Ninayo ahadi Yako, Wewe ulitoa ahadi Yako, ninawajua wengine walioponywa kwayo, nami nitashikilia papa hapa. Niko mikononi Mwako.” Amina. Jambo fulani litatukia basi.

⁸⁴ Unapochukua ahadi ya Mungu na kuishikilia, “Bwana, uliniambia ya kwamba kama ningetimiza masharti ya toba, na kadhalika, kwamba Wewe ungenipa ubatizo wa Roho Mtakatifu, niko papa hapa mikononi Mwako hata utakapofanya hivyo.”

⁸⁵ Ninapenda, kwa namna fulani, ushuhuda wa Buddy Robinson kule, alitoka akaenda katikati ya shamba la mahindi, akasema, “Usiponipa Roho Mtakatifu,” kasema, “utakaporudi duniani, kutakuwako na lundo la mifupa limewekwa papa hapa.” Nami napenda hilo. Naam, bwana. Hapo ndipo alipopata kitu fulani. Hivyo ndivyo unavyotaka kufanya. Lishikilie!

⁸⁶ Ninapendezwa na mwanamke huyo. Imani yake ilikuwa katika nabii, alimshikilia, akasema, “Sitakuacha.” Vema sana, ni ninii tu. . .

⁸⁷ Sasa, Yesu alifundisha jambo lilo hilo. Vipi kuhusu yule hakimu dhalimu na mjane? Yeye asingempa haki, ingawa alilia usiku na mchana, mbona, a—alimpatia haki na adui zake apate tu kumwondosha. Kasema, “Ni zaidi sana vipi Baba yenu wa Mbinguni atawapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?” Hilo ndilo tunalotaka.

⁸⁸ Usipoamini Roho Mtakatifu ni halisi, ishikilie ahadi ya Mungu, na udumu tu nayo, ishikilie, usiache. Kama huamini Yeye ni Mponya, ugonjwa wowote au shida uliyo nayo, sasa hivi, usiungojee mstari wa uponyaji, ishikilie tu sasa hivi, na useme, “Mungu, niko mikononi Mwako.”

Naye Shetani atasema, “Hujapata nafuu.”

⁸⁹ Hivyo ndivyo alivyoniambia, nikasema, “Angalia hapa, maskini mguu uliopinda, usiponini. . . kama ukitaka. . . ukitaka kunisikia nikishuhudia juu ya utukufu wa Mungu, subiri hapa, bali hutanitikisa niachane nayo. Kama ukitaka kusikia shuhuda za Mungu, na sifa za uponyaji wa Kiungu, simama karibu, nitautangaza kwa nguvu kwa muda mrefu tu niwezavyo, nidumu

tu moja kwa moja nao. Simama karibu, usikilize, ninakualika usikilize, kaa hapa.”

⁹⁰ Siku ya kwanza, hamna nafuu; kesho yake, hamna nafuu; kesho yake, hamna nafuu, niliendelea tu kukaa, nikishuhudia, nikimsifu Mungu, nikipenya katika mawingu meusi, Yeye alitoa ahadi, hatimaye, hiyo hapo. Baada ya kitambo kidogo anachoka na kutoroka.

⁹¹ Ndipo tunaona basi, ya kwamba nabii aliona asingeweza kumwondosha mikononi mwake, kwa hiyo akasema, “Vema, nitajikaza viuno, na hapa nitaambatana nawe.” Loo, jamani! Na kwa hiyo Gehazi alikutana nao akirudi. Imani yake . . . Sasa, hi—hiyo fimbo ingefanya kazi, lakini ni mahali imani yako ilipo. Kwa hiyo, imani yake haikuwa katika hiyo, ilikuwa katika nabii.

⁹² Kwa hiyo huyu hapa anakuja kule juu, huku wote wakiomboleza, na kupiga makelele, na kupiga mayowe, na matumaini yote yamekwisha, na kila kitu, ninaweza kumwazia akisema, “Shh, shh, shh, shh! Tulieni.”

⁹³ Atafanya nini? Nawatakeni mwone, aliingia chumbani ambamo mtoto huyo alikuwa amelazwa kitandani, akafunga mlango nyuma yake, yeye tu na huyo mtoto. Hizo ndizo nyakati za mafanikio zaidi, unapokuwa peke yako na Mungu. Unaona? Kuwa peke yako na Mungu.

⁹⁴ Yesu alisema, “Ingia katika chumba cha ndani na ufunge mlango. Mwombe Baba yako aonaye kwa siri, Yeye kwa wazi,” uh, “Atakufunulia waziwazi.”

⁹⁵ Kwa hiyo ninaweza kumwona huyo nabii. Sasa, Biblia ilisema alitembea huku na huku chumbani, akitembea tu. “Bwana, mimi hapa. Nifanye nini?” Akatembea huku na huko, alikuwa akimngojea Roho, baada ya kitambo kidogo akamgusa. Anaenda pale, na kuulaza mwili wake juu ya mwili wa huyo mtoto, akaanza kupata joto, akaamka na kuanza kutembea tena, akitembea huku na huku.

⁹⁶ Alihisi upako ukija mkubwa zaidi, kwa hiyo akaulaza mwili wake juu ya huyo mtoto mchanga, ndipo akapiga chafya mara saba. Akamchukua, akamtoa nje, akamkabidhi mama yake.

⁹⁷ Loo, jinsi maskini Bartimayo alivyoipenda hadithi hiyo! Angesema . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁹⁸ “Mnaona, Mungu hana budi kutimiza kusudi Lake, Bartimayo. Mnaona? Mungu hana budi kufanya jambo fulani, kumleta mtu fulani kwa ajili ya jambo fulani, Yeye huagiza mambo.”

“Loo, Mama, wewe ni mrembo sana, naam, ninakupenda tu, Mama.”

⁹⁹ “Nawe unajua, Bartimayo, kabla hujazaliwa, huelewi sasa, Mpenzi, lakini kabla hujazaliwa, nilikuweka wakfu kwa Mungu,

kwa Yehova. Unajua nini? Haitanishangaza hata kidogo, ila macho yako madogo yatamwona Masihi.”

Naye akawaza, “Loo, ole, laiti angelikuja sasa, mimi ni kipofu!”

“Lakini unajua, Bartimayo, Mungu huwatumia wavulana wadogo kwa ajili ya utukufu Wake. Yeye ana kusudi, nami ninaamini Yeye ana kusudi fulani maishani kwa ajili yako.”

¹⁰⁰ Ndipo, alipowazia hilo, “Loo, isingewezekana sasa, angalia ilivyokuwa. Maskini huyo mama, aliomba, ameondoka miaka mingi iliyopita. Lakini nadhani kile alichoombea kilipotea.” Mwajua, juu ya hayo mango. . .

¹⁰¹ La, la. Hakuna maombi maaminifu yaliyowahi kufanywa, ila ambayo yanajibiwa. Nina umri wa miaka hamsini na mmoja, nami nimekuwa katika huduma miaka thelathini na mmoja, nami nitasema mbele ya Biblia ya Mungu, kamwe sikuomba chochote kwa uaminifu, pasipo Mungu kunipa, ama kuniambia sababu ya Yeye kutoweza kunipa. Ninasema hivyo kama mtumishi wa Kristo. Hiyo ni kweli. Kati ya mara makumi ya maelfu ambayo nimemwomba Yeye vitu, kumwomba chochote kwa uaminifu, kuchukua, kutaja kitu kimoja na kumwomba Yeye, ama angeniambia. . . Yeye angenipa, ama kuniambia ni kwa nini asingeweza. Kwa hiyo ninajua daima ni bora zaidi ikiwa siwezi kupewa.

¹⁰² Maskini mtoto wako wa kiume angekuomba wembe wako kunyoa nao, ungekuwa baba duni kumpa, angejidhuru. Anajua yaliyo mema kwetu, na yale yasiyofaa.

¹⁰³ Kwa hiyo, basi Bartimayo angewazia hivi: “Unajua nini? Chini kidogo tu hapa kuna kivuko ambapo Israeli walivukia. Basi wazia tu, moja kwa moja kwenye barabara ii hii ambapo kasisi huyo alipitia muda mfupi uliopita, yule nabii mashuhuri Eliya pamoja na Elisha walikuja wameshikana mikono kwenye barabara hiyo, wakishuka kwa miguu kwenda Yordani kuifungua tena.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁰⁴ Basi, tangu wakati Israeli walipovuka mpaka yule nabii mkuu, Eliya, Mungu alinena na kuifungua bahari, aliweza kuyafungua hayo maji. Akawazia, “Loo, laiti ningaliishi tu katika siku hiyo! Hao manabii wawili wakuu wameshikana mikono, wakishuka kwenda Yordani, mmoja wao alikuwa anarudi, huyo mwingine alikuwa anaenda juu. Huyo mzee alikuwa amepigana na Yezebeli na Ahabu, na dhambi za ulimwengu, na ng'ambo tu ya mto kulikuwako na farasi aliyekuwa amefungwa pale kwenye kichaka fulani, na gari la Moto lilikuwa limchukue kumpeleka Utukufuni; huyo nabii kijana anaenda kupokea sehemu maradufu kwa ajili ya huduma yake kurudi, wanatembea wameshikana mikono.”

105 Akasema, “Laiti ningalikuwa nimeketi kwenye mwamba huu wakati huo, ningetoka mbio na...” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

106 “...kwa sababu wewe ni mtu ambaye humleta Mungu, dhahiri, kwa watu. Mwombe tu Yehova, nami nitapata kuona.’ Lakini kuhani ananiambia ya kwamba watu hao wote... Yehova aliacha kufanya hivyo miaka mingi iliyopita.” Wangali wanawazia jambo lile lile, bali Yeye anaendelea vivyo hivyo, tu, naam, angali ni Yehova.

107 Ninafikiri aliwazia, “Kama ningaliweza kutoka kwenda huko nje na kusimama, mbona, ni, hao manabii, hakika wangenibariki, nami ningepata u—uponyaji. Lakini yote yamekwisha sasa, siku za miujiza zimepita, kwa hiyo hakuna kitu ninachoweza kufanya juu yake, nadhani, ila kuketi tu hapa kipofu.”

108 Upepo ukavuma, naye akajifunika...akajifunika kwenye koti lake, ndipo akaanza kuwazia juu ya hadithi nyingine, yule Yoshua mkuu siku moja. Si zaidi ya yadi mia moja ama mbili kutoka mahali alipokuwa ameketi, Israeli walivuka mto huo wenye nguvu kwa yule mtawala mkuu, Yoshua.

109 Kisha akakumbuka hadithi nyingine, kwamba walipokuwa wamepiga kambi huko nje, Israeli, Nguzo kuu ya Moto ya Mungu ikining’inia juu yao, siku moja Yoshua, yule jemadari mkuu, alitoka akaenda kuangalia ninii yake, kupata ninii yake, mbinu ya kuzibomoa hizo kuta na kuziondolea mbali, Yeriko. Alipokuwa akitembeatembea, alimwona Mtu fulani akienda kukutana naye, alikuwa ni Shujaa mwingine. Yoshua aliuchomoa upanga wake, kwa sababu alikuwa mpiganaji, upesi akainua upanga wake juu, na kusema, “Je, Wewe u upande wetu, au uko upande wa adui yetu?”

110 Ndipo Jamaa huyo mkuu akauchomoa upanga Wake, nayo radi ikaruka kutoka nchani mwake, akasema, “Mimi ni Amiri jeshi wa jeshi la Bwana. Mimi ni Amiri jeshi wa Bwana.”

111 Yoshua mkuu, mwenye nguvu akatupa chini ngao yake, akatupa chini upanga wake, akatoa chapeo yake, akasujudu miguuni Pake.

112 Loo, huenda alisema, “Kama ningaliishi katika siku hizo ningetaka kusujudu miguuni Pake, pia.” Lakini hakujua ya kwamba Amiri jeshi yeye yule wa jeshi la Bwana, si yadi mia moja kutoka kwake, Amiri jeshi yeye yule, wakati alipokuwa akiwazia juu ya mambo hayo.

113 Kwa kawaida ni wakati unapowazia juu ya Bwana, kwa kawaida ni wakati umeweka mawazo yako, si kwenye jambo lingine, mambo ya ulimwengu, ama jinsi utakavyopata pesa nyingi sana, ama ni dhehebu kubwa namna gani utakalojenga...

114 Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu siku hizi, tumeweka mawazo yetu juu ya mambo ya ulimwengu badala ya kumwazia Mungu, hebu tumwazie Mungu. Biblia ilisema, “Kukiweko na sifa yoyote, kukiwepo wema wowote, yatafakarini mambo haya.” Akili zetu hutangatanga, na muda si muda mwajua, tumepotelea huko nje mahali fulani, tunawazia juu ya jambo lingine. Hebu nimweke Yesu moyoni mwangu, niani mwangu siku nzima, mchana na usiku. Hiyo ndiyo njia.

115 Alipokuwa akiwazia hayo, alisikia kelele. Ni ajabu, popote alipo Yesu kuna kelele nyingi. Sijui ni kwa nini, lakini kwa kawaida ndivyo ilivyo. Ndipo kelele nyingi zikatokea upande wa ndani. Jambo la kwanza, lango likafunguka, akasikia kelele nyingi, na watu wakikimbia, na wengine wakipiga mayowe, “Hosana, Hosana kwa Nabii wa Galilaya!” Wanawake, na baadhi ya wanaume.

116 Ndipo angeweza kusikia wengine wakipiga makelele, na kumdhihaki, “Wewe si kitu ila bandia!” Alitupiiwa mayai na matunda yaliyooza.

117 Akamsikia kasisi yuyo huyo, muda mfupi hapo kabla, kabla lile shirika halijakutana, “Aisee, unasema ati wewe ni nabii, tulisikia ya kwamba ulimfufua mtu aliyekufa kutoka kaburini. Tunakujua, laghai! Walimplaza mtu huyo mle, nao wanafunzi wako wakafanya hivyo, huyo si kitu ila ni bandia. Kama unaweza kuwafufua wafu, tuna makaburi yaliyojaa hao hapa juu, njoo, ukawafufue baadhi yao, tutakuamini.”

118 Yesu hamjali ibilisi, kamwe hakumjali. Maskini ibilisi yuyo huyo alimwambia wakati mmoja, “Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yageuke kuwa mkate.” Angeweza kufanya hivyo.

119 Mmoja wao alimfunga kitambaa usoni Mwake siku moja huko chini nyuani, akakizungushia usoni Mwake, machoni Mwake, na kumpiga kichwani kwa fimbo, hao wenye kudhihaki, na kusema, “Ikiwa wewe ni nabii twambie ni nani aliyekupiga.” Mnamwona ibilisi huyo wa kale?

120 Ibilisi yuyo huyo wa kale yu hai leo, “Shuka uje hapa chini ukamponye mzee *Nanii* pale pembeni. Nenda hapa kwa *nanii*, ukawaponye.”

121 Hatuchukui amri kutoka kwa ibilisi. Yesu alisema, “Siwezi kufanya lolote mpaka Baba anionyeshe kwanza la kufanya. Kwa kuwa Yeye anatenda kazi, nami ninatenda kazi hata sasa.” Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

122 Kwa hiyo ukimsikia mtu yeyote akisema jambo kama hilo, mwondokee, ni ibilisi. Hatuchukui amri kutoka kwa Shetani. Ndio kwanza tutoke Juu, wakati Yeye anapotuonyesha la kufanya, basi tunaenda kulifanya. Kama anataka Bw. Jones pale pembeni aponywe, atamwambia mtumishi Wake, naye ataenda kule na kumponya, mnaona, hiyo ni kweli, kwa amri Zake tu.

“Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe kwanza la kufanya,” Yohana Mtakatifu 5:19.

¹²³ Sasa, ninaweza kumsikia kasisi huyo akimwita, “Wewe si kitu ila bandia!”

¹²⁴ Yesu, huku mizigo na dhambi za ulimwengu zikiwa juu Yake, alikuwa anaenda moja kwa moja Kalvari, moja kwa moja mpaka Yerusalemu apate kukabidhiwa mikononi mwa watu wenye dhambi, Mataifa, walikuwa wamsulubishe. Mizigo yote na dhambi ya, kila dhambi iliyopata kutendwa duniani, ama itakayopata kutendwa, ilimkalia Yeye.

¹²⁵ Nao walikuwa wakicheka, wakimdhihakiki; wengine wakipaza sauti, “Hosana kwa Nabii wa Galilaya, Mwana wa Daudi!”

¹²⁶ Hivyo ndivyo ilivyo leo mumu humu Beaumont, Texas. Baadhi yao watacheka na kufanya mzaha, wengine wanaiamini hiyo hadithi. Daima imekuwa hivyo, na daima itakuwa hivyo, mpaka ukomo, itakuwa hivyo, umati uliochanganyikana.

¹²⁷ Kila uamsho huzaa mapacha. Wale wana wawili wa Yakobo, ama, Isaka wamewakilishwa vizuri. Kila wakati kunapokuwa na uamsho, kuna Esau anayezaliwa na Yakobo anayezaliwa: Mtu mmoja wa kidini wa ulimwengu anakuwa mgumu, na kuchukua ujuzi fulani wa seminari, huku huyo mwingine anataka haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza haidhuru ataipataje. Kama ikimbidi kuwa mtakatifu anayejibingirisha, ama chochote kile, anataka hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza, sijali.

¹²⁸ Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, wanaogopa hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza. Loo, jinsi ambavyo wanaichukia hiyo! Lakini inazaa mapacha. Watu wa ulimwengu, wanaoegemea kwenye dini sana, wanatoa sadaka nzuri, na kadhalika, bali kamwe hawajali kuhusu hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza.

¹²⁹ Makundi hayo mawili makubwa yamekuwa yakipigana tangu ulimwengu ulipoanza, nao wako karibu kufika kwenye kichwa sasa hivi ambapo, jambo ambalo Yesu alisema, wangepanana sana, wangepoteza walio Wateule kama yamkini. Ni kweli. Mnaona ni saa ya udanganyifu jinsi gani tunayoishi.

¹³⁰ Dumu pamoja na Neno, ndugu, usiliache hilo Neno. Hiyo ni kweli. Neno litajitetea Lenyewe.

¹³¹ Ndipo ninaweza kumwazia maskini Bartimayo akijaribu kusimama, akisema, “Haya yote yanahusu nini?”

“Keti chini!”

“Hizo kelele ni za nini? Ati nini? Ni nani amefanya jambo fulani?”

¹³² Hakuna mtu angemsaidia; alikuwa kipofu. Ninachukia kuona jambo hilo, kumsukuma tu maskini kipofu huku na huku.

Ndipo muda si muda mwajua, hapana shaka kulikuwa na ninii, nitawazia, msichana mmoja akapitia hapo, naye maskini huyo jamaa alikuwa amesukumwa nyuma, naye alikuwa akijaribu kusimama kwa magoti yake katika maskini matambara yake, yeye akamsaidia kusimama vizuri na kwa upole. Akasema, “Bwana, naona kwamba wewe ni kipofu.”

“Naam, mama. Wewe ni mwema sana kwa vipofu.”

“Naam, ninamhurumia kipofu, au mtu yeyote mhitaji.”

133 “Mama, waweza kuniambia, hakuna mtu atakayeniambia, kelele hizo ni za nini? Nimekuwa hapa kwa miaka mingi, sijawahi kusikia ke—kelele kama hizo. Kila mtu anasema jambo moja, na mwingine *lingine*.”

“Loo, bwana! Hivi hujapata kujua ya kwamba Yesu wa Nazareti, yule Nabii, anapitia hapa?”

“Ati nani?”

“Yesu wa Nazareti.”

“Mbona, Yesu wa Nazareti ni Nani?”

“Wewe ni Myahudi, sivyo?”

“Loo, naam.”

134 “Vema, uliwahi kujua katika Maandiko ya kwamba—ya kwamba Bwana Mungu wetu atainua Nabii kama Musa, Naye atakuwa Masihi?”

“Loo, naam. Nilikuwa tu nikiwazia hilo, nilikuwa tu nikiliwazia. Loo, naam, Yeye atakuwa ni Mwana wa Daudi.”

“Vema, huyo Ndiye anayepita hapa!”

“Jina Lake ni nani?”

135 “Yesu wa Nazareti, Yeye ndiye Masihi. Nilimwona akiwapa vipofu kuona. Loo, laiti ungalimwona asubuhi ya leo! Bila shaka alithibitisha Umasihi Wake wakati alipokuja upande wa kusini mwa mji. Laiti ungalimwona! Je, unamkumbuka maskini jamaa mmoja mjini hapa jina lake Zakayo?”

“Loo, naam, mume wa Rebekah.”

“Naam.”

“Amenipa sadaka mara nyingi, yeye ni mfanyabiashara.”

136 “Um-hum. Vema, kwa namna fulani alikuwa mdogo wa kimo, wajua. Naye Rebekah amekuwa akihudhuria huo mkutano. Nami ni mwanafunzi wa huyu Bwana Yesu, nasi tumefundishwa kama Wakristo, wanafunzi Wake, kuheshimu na kuwa wafadhili na wakweli.” Hiyo ni kusema, Wakristo wote hufanya hivyo, wanaonyesha heshima, mnaona. “Na hiyo ndiyo sababu nataka ufahamu, bwana. Na asubuhi ya leo nilikuwepo, kwa kuwa tulijua Yeye alikuwa anakuja. Naye Rebekah alikuwa ameomba kwa muda mrefu sana kwamba Zakayo. . .

¹³⁷ “Yeye ni mtu mzuri, lakini kwa namna fulani anajigamba, kwa sababu anaegemea sana kwenye sinagogi. Nanyi mnamjua Rabi Kavinski, kule, yeye—yeye kwa kweli hampendi Yesu wa Nazareti, nao walikuwa na shirika la wahudumu hapa, basi wakakutana asubuhi ya leo na kumzuia Yesu kufanya miujiza mjini, wakamfukuza, kwa hiyo akaondoka tu.

¹³⁸ “Lakini mnajua, Rebeka alikuwa ameomba kwa bidii sana kwamba Zakayo angekuja kumwamini Bwana Yesu kama Masihi wa Mungu, naye alikuwa amemwambia mambo yote ambayo Masihi alifanya, na jinsi ambavyo angekuwa Mfunuzi wa siri za moyo, na kadhalika.

¹³⁹ “Unajua Zakayo alifanya nini? Kwa namna fulani alikuwa mfupi wa kimo, kwa hiyo alikuwa huko chini langoni mapema sana,” ambapo tunajua ingekuwa. “Na unajua, alipoona atakuwa mfupi sana asiweze kumwona, kwa hiyo nina hakika... Mimi na Rebeka tulikuwa tumefanya agano, sisi kwa sisi, tulikuwa tunaenda kuomba kwamba kama Masihi angekuwa... angekuwa... angemtambua Masihi.

¹⁴⁰ “Kwa hiyo nikamwangalia Zakayo, akakimbia chini *kabisa* kwenye Barabara ya Haleluya akaja kwenye Barabara ya Utukufu. Basi unajua hiyo mikuyu inayosimama pale?” Kwa maneno mengine, kulikuwa na mitende. Kasema, “Alipanda juu pale, naye akasema, ‘Sasa, nitajipatia mahali pa kuketi papa hapa kwenye tawi lililogawanyika. Nitaketi chini, niweke mguu mmoja upande *huu*, na mmoja upande *huu*, nitamtazama atakapopiga kona, maana Yeye sikuzote hufuata Barabara Kuu ya Haleluya na Barabara ya Utukufu. Sikuzote hudumu mumo humo, kwa hiyo ninajua nitakutana Naye kule.’ Kwa hiyo akaketi mahali ambapo matawi mawili yalikutana.”

¹⁴¹ Sasa, hapo ndipo watu wengi wanapoketi usiku wa leo, ambapo njia yako na njia ya Mungu hukutana, uamuzi lazima ufanywe. Huenda ukawa hapa usiku wa leo katika hali iyo hiyo.

¹⁴² “Vema, akaanza kuwazia kule juu, alitwambia muda mfupi uliopita baada ya kile kilichotukia, kilichotukia. Kwa hiyo shirika la wahudumu halingemruhusu aende kwenye jumba la mikutano kufanya mkutano, kwa hiyo, ambao Yeye alikuwa anaenda kuwa nao. Kwa hiyo Zakayo, akapanda juu ya mti, akasema, ‘Rebekah aliniambia ya kwamba Mtu huyu angeweza kuyatambua mawazo ya moyo. Sasa, siamini katika... Rabi Kavinski, mchungaji wangu, aliniambia ya kwamba jambo hilo halikutukia tena.’”

¹⁴³ Kama kuna Rabi Kavinski hapa, samahani. Ninatumia tu hili kwa... Mnaona? Ama ningeweza kusema mzee wa jimbo, ama kitu kama hicho, ama msimamizi wa wilaya, ama mwajua, chochote tu kitafaa, namna hiyo. Mnajua ninakoelekea. “Kwa hiyo basi, kwa vyovyote vile, anapanda juu ya mti, naye...” Ama Daktari, Ph.D., LL.D., ama yoyote ya hizo, mwajua.

144 “Kwa hiyo anapanda juu ya mti, akasema, ‘Unajua nini? Nitahakikisha kwamba Jamaa huyo hajui lolote kunihusu mimi.’ Kwa hiyo akashika majani yote na kujifunika nayo, akajificha.” Alikuwa ni jamaa mdogo, kwa vyovyote vile, ameketi juu ya tawi hili, mwajua, namna *hii*. “Kwa hiyo akaacha jani moja dogo pale, ambalo yeye, kama mlango, angeweza kuangalia juu na kumwona Yeye alipopiga kona kwenye Barabara Kuu ya Haleluya, akipanda kwenye Barabara ya Utukufu, maana ilikuwa karibu sana pale pembeni. Basi baada ya kitambo kidogo, wakati ameketi pale,” akasema, “laiti ungalimsikia akishuhudia jambo hilo, bwana!”

145 Yesu alikuwa akipita. Naye maskini huyo kipofu alikuwa akisikiliza hiyo hadithi, maana alijua kile mama yake alichomwambia ya kwamba Masihi angekuwa, kwa hiyo anasikiliza hadithi hii. Yesu alikuwa anaendelea, walikuwa wakimtupia vitu, na kumdhihaki, na kumwambia, njoo ukawafufue wafu, kwamba wangeona hakuna udanganyifu ndani yake, na kadhalika namna hiyo. Na—na kwa hiyo, wakati wao . . .

146 Kasema, “Naye alitwambia basi kwamba alijificha chini ya majani haya, kisha akauacha mlango huu mdogo wazi. Ndipo wakati—wakati . . . Unajua nini? Kasema, ‘Atakapopitia hapa, nitachungulia tu na kumtazama.’ Kasema, ‘Kwa sababu wengine wote walikuwa wakimwangukia, mbona kwa ajili ya fahari, nitamtazama tu.’ Kwa hiyo akajificha, asiye akamwona.”

147 “Kwa hiyo akainua kifuniko, na baada ya kitambo kidogo huyu hapa Yesu anakuja, na mwanamke akijitokeza, na mtume mkubwa mno akitangulia, Simoni Petro, pamoja na wengine kumi na mmoja, wakisema, ‘Samahani, Nabii amechoka sana, hatuna budi kumpeleka mbele sasa. Yeye—Yeye kwa namna fulani . . . hakuweza kufanya mkutano kule chini, kwa hiyo inatubidi kurudi nje ya mji.”

148 Kisha kasema, “Alimwangukia kwa dakika chache, Naye akaja moja kwa moja hapo, akainua kifuniko zaidi kidogo na kuchungulia, kasema, ‘Unajua, kwa namna fulani napenda sura ya Jamaa huyo.’” Kuna *kitu fulani*, kamwe huwezi kumwangukia Yesu moja kwa moja na kamwe ujisikie vivyo hivyo tena, *jambo fulani* kulihusu, Yeye atakushika.

149 “Kwa hiyo akainua jani lake dogo namna *hii*, na kuliinua, na kusema, ‘Huh! Hakika nilimpumbaza wakati huu, nikapanda juu ya mti. Na ati huyo ndiye Jamaa anayejuu siri za moyo? Huh! Vema, Yeye—Yeye huenda akawa ni Nabii, nijuavyo mimi.’ Naye anafika huku *hivi*.

150 “Akasimama moja kwa moja chini ya mti, akaangalia juu na kusema, ‘Zakayo, shuka chini.’ Si kwamba tu Yeye alijua alikuwa kwenye mti, alijua jina lake.”

¹⁵¹ “Loo,” Bartimayo akasema, “huyo ni Yeye! Huyo ni Mwana wa Daudi! Loo, Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!” Huyo hapo anaenda, katika umati wa elfu moja, labda watu elfu saba ama elfu nane, wakipigia mayowe jambo *moja*, na *lingine*, “Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Nirehemu! Ninaamini ya kwamba Wewe ni Nabii aliyekuwa aje. Ee Mwana wa Daudi!”

¹⁵² Sasa, asingeweza kumgusa Yeye. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ningeweza kuhubiri juu ya hilo kwa urahisi sana. Loo, jinsi imani katika Mungu itakavyofanya! Nani? Hana budi kuwa askofu? Mkuu wa wilaya? Daktari LL.D. Jones? La, bwana. Ombaomba, amechakaa, kipofu, bali alikuwa na imani ya kutosha.

¹⁵³ Angalia mzigo ulio juu Yake, huku yote yakimkabili, hapana shaka ila kwenye nguo Zake kulikuwa na uvundo wa matunda yaliyooza, na vitu walivyokuwa navyo, mboga, walizokuwa wamemtupia, lakini alikuwa na akili timamu, alikuwa ameelekea Kalvari. Ulimwengu mzima ulikuwa umewekwa mabegani Mwake, lakini imani ya ombaomba kipofu ilimsimamisha na kumfanya kusimama kimya. Amina.

¹⁵⁴ Jeshi lile lile lenye nguvu la Bwana lililolisimamisha jua kwa ajili ya Yoshua. Yoshua alisimamisha j-u-a kwa imani, lakini Bartimayo kipofu alimsimamisha M-w-a-n-a kwa imani. Na imani iyo hiyo itamleta kutoka Utukufuni, ambako Yeye hutawala mfumo wa jua, na ulimwengu, itamleta kwenye maskani hii usiku wa leo, imani ile ile kama ya mtoto.

¹⁵⁵ Akasimama na kusimama kimya, akaangalia kote. Wakamleta huko. Akasema, “Imani yako imekuponya.” Huh! Loo, jamani!

Huyo hapo aliendelea kutembea, maskini mama huyo amemshika mkono, hapana shaka alisema, “Je, ulisikia aliyosema?”

“Loo, naam! Loo, wazia, Yeye aliniambia ningepata kuona.”

¹⁵⁶ Msafara ulikuwa ukishuka barabarani, Yeye alikuwa akielekea mlimani aende akasulubiwe. Akasema, “Upate kuona, imani yako imekuokoa.”

¹⁵⁷ Kama vile tu imani yako inavyokuokoa na kuzimu, neno lile lile la Kiyunani linatumiwa, *Sozo*. Naam, lile lile, kila wakati linapotafsiriwa, kuokolewa kimwili, ama kuokolewa kiroho, imani ile ile hufanya jambo lile lile. “Imani yako imekuokoa.”

¹⁵⁸ Loo, imani yake ilimsimamisha Yesu, na kumfanya asimame kimya. Kwa hiyo, akasema, “Aliniambia! Yeye ndiye Masihi. Alikuwa na . . . Yeye ana ishara zote za Masihi, Naye aliniambia nitapata kuona, nimeridhika nitapata. Loo, nimeridhika! Nimeridhika!” Anaanza kusema.

Mara akaona kivuli, “Huh! Loo, nimefunguliwa macho!” Naye huyo akashuka barabarani.

159 Anaposema jambo lolote, endelea tu kuliadini.

160 Nilisoma hadithi ndogo, huenda ikawa ni hadithi ya kubuniwa, labda sivyo, sijui, juu ya Bartimayo, ilisema alikuwa na mke na msichana mdogo. Nayo ikasema kwamba usiku mmoja mke wake alikuwa mgonjwa, kwa hiyo a—akatoka nje, akasema, “Yehova, kitu pekee nilicho nacho cha kukutolea Wewe...”

161 Iliwabidi kuwa na namna fulani ya burudani kuvutia usikivu, ombaomba walikuwa nayo, kama wafanyavyo huko India. Kama ombaomba huko India hana kitu cha kuvutia usikivu wa—wa mpita njia, kamwe hatapata sarafu, atapata kwa nadra, kwa vyovyote vile. Wana tumbili wadogo, maskini tumbili huyo atampiga jamaa huyo, naye atakimbia kana kwamba anapiga mayowe na kulia. Wana swila, nyoka, anayepigana na m—mnyama mdogo, nao... na kila kitu cha kuburudisha, *kitu fulani* cha kuwafanya watoe sarafu.

162 Kwa hiyo, walisema ya kwamba Bartimayo alikuwa na hua wawili wadogo, wangefanya sarakasi mmoja na mwenzake. Akasema, “Yehova, sina mengi, lakini kama utamwacha tu mke wangu aishi, tabibu ndio kwanza aondoke na kusema atakufa, ninamhitaji sana, kama utamruhusu tu aishi, kesho asubuhi nitakupa hua wangu wawili kama dhabihu.”

163 Ndipo mke wake akapata afya, kwa hiyo akawatoa dhabihu hao hua. Majuma kadhaa baadaye, yeye... kasema alikuwa na msichana mdogo ambaye hakuwa amewahi kumwona maishani mwake, msichana mdogo, mwenye nywele za kipilipili. Usiku mmoja alishikwa na ugonjwa mbaya sana, ndipo yule tabibu mwema akaja tena, akasema, “Bartimayo, huyu mtoto karibu apate mipagao, nafikiri mtoto huyo atakufa.”

“Loo,” akasema, “Tabibu mwema, una hakika?”

164 “Kadiri mafunzo yangu ya matibabu yanavyonijulisha, mtoto huyo yuafa sasa. Homa zinaingia katika kifafa, wala hakuna kitu kinachoweza kufanywa kwa ajili yake.”

165 Ndipo akatoka nje, kando ya nyumba kwenye mwangaza wa mbalamwezi, akipapasa-papasa kando, akasema, “Yehova, sina ila kitu kimoja kilichosalia.”

166 Sijui wanamwita mbwa wa aina gani siku hizi, anayewaongoza vipofu, Ninasahau. [Ndugu fulani anasema, “Mbwa wa jicho-lionalo.”—Mh.] Mbwa wa jicho lionalo. Vema, badala ya m—mbwa kumwongoza kipofu katika siku hiyo, walikuwa na mwana-kondoo ambaye angemwongoza kipofu.

167 Kwa hiyo Bartimayo, walisema, alikuwa na mwa—mwana-kondoo aliyemwongoza, akasema, “Huyo ndiye yote niliyo nayo ya kutoa, Yehova, lakini ninampenda sana msichana wangu mdogo, endapo utamjalila tu apone wala asife, kesho nitaenda

he—hekaluni, nami nita—nitakupa Mwana-kondoo huyo kwa ajili ya dhabihu.”

¹⁶⁸ Huyo msichana mdogo akapata afya. Kesho yake asubuhi, alikuwa njiani mwake akimpeleka huyo mwa—mwana-kondoo kwenye dhabihu. Nayo ikasema kuhani alitoka nje, na kusema, “Kwani unaenda wapi, Bartimayo?”

¹⁶⁹ Akasema, “Loo, Kuhani, mtumishi wa Mungu, ninapanda kwenda hekaluni kutoa mwana-kondoo wangu kwa ajili ya dhabihu.” Akamwambia hadithi ya msichana wake mdogo kuwa mgonjwa, na kusema, “Nilimtolea Yehova, alipomponya mke wangu, nilitoa wale njiwa, ndipo wakati msichana wangu mdogo alipopona, nikamwambia ningempa huyu mwana-kondoo.”

¹⁷⁰ Akasema, “Loo, Bartimayo, huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo! Haya, nitakupa pesa, nawe ujinunulie mwana-kondoo kutoka kwa wabadilishaji huko nje, yale mazizi. Wewe nunua mwana-kondoo, nitakupa pesa za kumnunua.”

¹⁷¹ Akasema, “Loo, Kuhani, hilo ni jambo zuri sana kwako, bali kamwe sikumwahidi Yehova mwana-kondoo *yeyote*, nilimwahidi Mwana-kondoo *huyu*.” Haya basi, ndugu. Nina hakika mnapata matumizi ya kiroho hapo. “Kamwe sikumwahidi mwana-kondoo *yeyote*, nilimwahidi mwana-kondoo *huyu*.”

“Mbona,” akasema, “Bartimayo, huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo, huyo mwana-kondoo ndiye macho yako!”

¹⁷² Akasema, “Loo, kuhani, kama nitakuwa mwaminifu kwa ahadi yangu kwa Yehova, Yehova atatoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo.” Hivyo ndivyo alivyofanya, alitoa Mwana-kondoo. Katika asubuhi hii yenye baridi, ya majira ya kuchipua, Yehova alikuwa ametoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu.

¹⁷³ Hebu niseme jambo hili kwa kusanyiko langu linalongojea usiku wa leo: Mwana-kondoo yuyo huyo ametolewa kwa ajili yenu usiku wa leo. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” Nayo imani yetu, usiku wa leo, inaweza kumleta Mwana-kondoo yuyo huyo wa Mungu moja kwa moja miongoni mwetu kufanya miujiza ile ile na ishara alizofanya kabla ya Yeriko, na hao wengine. Mnaamini hilo?

Na tuombe.

¹⁷⁴ Ee Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi za ulimwengu, naja Kwako sasa kwa moyo wangu wote kwa ajili ya watu hawa wagonjwa. Wanangojea kwa saburi, wengi wao wakisimama, viungo vyao vinauma, bali Wewe ni Mungu, utawapa thawabu.

¹⁷⁵ Wanazo, zimewekwa hapa, lesu na vifurushi vidogo vya vitambaa, ninaweka mwili wangu juu yavyo katika Jina la

Bwana Yesu, nikiomba ya kwamba utazituma nguvu Zako na baraka pamoja nazo, kumponya kila mgonjwa ambaye hivi vilimwakilisha, kwa yule mtoto mchanga mwenye homa anayekingojea *hiki*, kwa maskini yule baba kipofu aliyeketi pale usiku wa leo katika ile nyumba ndogo huku ule mkongojo mweupe ukiugonga mlango. Ee Yehova, nenda upitie katikati kule, Bwana, ukawaponye; Wewe ni Mungu.

¹⁷⁶ Kuna wengi huko katika...hospitalini wakingojea, mgonjwa akifa, matumaini yote yamekwisha; Wewe ungali ni Yehova Mungu. Wasingeweza kuja mkutanoni, ila Wewe unaweza kwenda mahali walipo, Baba. Ninaomba ya kwamba utatujalia hivyo.

¹⁷⁷ Ninaomba ya kwamba rehema Zako zikae juu ya watu sasa. Jalia uponyaji wa kila mgonjwa aliye hapa, wokovu kwa kila nafsi iliyopotea, ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa kila mwaminio, kusudi mkutano huu uweze kumalizika katika upeo mkuu huku Mwana-kondoo wa Mungu akiwaongoza katika njia za haki, kwenye zile chemchemi kuu za uponyaji wa rehema ya Mungu, kwenye vile vidimbwi vikuu vya wokovu wa Roho Wake Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

¹⁷⁸ Ninawakabidhi Kwako sasa, pamoja nami, ili upate kujionyesha Mwenyewe kwamba imani yetu usiku wa leo, kama yule ombaomba kipofu ambaye ndio kwanza tuzungumze habari zake, anavyoweza kuuleta Uwepo wa Mwana-kondoo wa Mungu miongoni mwetu kuonyesha ishara zile zile alizofanya alipokuwa hapa. Na watu wote watakuamini, Baba, na—natumaini kwa moyo wangu wote, ninapokabidhi sisi Kwako, tukimngojea Roho Wako kulithibitisha Neno ambalo limehubiriwa kwa ishara zinazofuata. Amina.

Nampenda,

Mwabuduni sasa.

Nampenda,

Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

Loo, Yeye si ni wa ajabu? Hebu tuinue tu mikono yetu usiku wa leo, tuuvumishe tu.

Sasa peana mikono na msafiri aliye karibu nawe, mahali fulani.

Na...

...kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,

Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu

Mwenye Nguvu;

Huniokoa, hunilinda na dhambi zote na aibu,

Mkombozi wangu ni wa ajabu, lisifu Jina Lake!

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Loo, Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, huniokoa, hunilinda na dhambi zote na aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, lisifu Jina Lake!

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa nimepatikana, huru na hukumu,
Yesu anatoa uhuru na wokovu mkamilifu;
Huniokoa, hunilinda na dhambi zote na aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, sifu . . .

Loo, hebu tuinue tu mikono yetu tunapouimba.

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, huniokoa, hunilinda na dhambi zote na aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, lisifu Jina Lake!

¹⁷⁹ Loo, hivi Yeye hakufanyi ujisikie vizuri? Jamani, ni hisia ya jinsi gani! Mnajua ni kwa nini nimewafanya muimbe? Ninapenda kuimba. Hivi hampendi kuimba? Baada ya ujumbe, unajisikia tu kama Neno la Mungu lina—linakusugua tu. Mnaona? Na halafu napenda uimbaji mzuri wa kale wa Kipentekoste. Nachukia sauti iliyofunzwa kupita kiasi, huko si kuimba, kushikilia pumzi yako mpaka unageuka samawati usoni, na, unaigiza tu basi. Ninapenda tu ule uimbaji mzuri, wa mtindo wa kale. Loo, jamani! Ninapenda:

Yesu ni wa ajabu, wa ajabu kwangu,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, huniokoa, hunilinda na dhambi zote na aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, lisifu Jina Lake!

Yeye si ni wa ajabu? Mwajua, kumekuwako na wimbo mmoja ninaopenda kuimba daima, huo ulikuwa *Hakuna Kitu Kati Ya Nafsi Yangu Na Mwokozi*.

¹⁸⁰ Wala kamwe nisingeweza kuimba, nisingeweza kuimba hata kidogo. Lakini moja ya siku hizi wakati nyote mtakapofika kwenye jumba lenu kubwa la kifalme Mbinguni, nitawapa ufahamu kidogo wa jambo fulani, na kote chini, huko chini kabisa, unaposimama kwenye mlango wako mkubwa wa ikulu, ukitoka asubuhi moja, huko chini *kabisa*, na karibu na mahali

pale ule Mto unapopiga kona baada ya kutoka kwenye kiti cha enzi cha Utukufu, mwajua, kuna msitu mdogo umewekwa pale, na kuna kibanda kidogo cha magogo, hicho ni changu, halafu basi, u—utakapofika huko chini asubuhi moja, ukitembea kwenye baraza lako, utege masikio, ukisimama pale chini kwenye ukumbi huo wa kale. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “...Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana, nilikuwa kipofu lakini sasa ninaona.”

¹⁸¹ Unajua kile ninachotaka useme? “Mungu asifiwe, maskini Ndugu Branham alifaulu! Huyu hapo, papo hapo chini sasa.” Naam, bwana. Loo!

Wakati tumekuwa huko miaka elfu kumi,
Tukiangaza kama jua;
Hatutakuwa na siku pungufu za kuimba sifa
Zake
Kuliko wakati tulipoanza mara ya kwanza.

Hebu tuuimbe, kila mtu.

Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu,
Iliyomwoko mwovu kama mimi!
Wakati mmoja mimi. . . [Sehemu tupu
kwenye kanda—Mh.] . . . nimepotea, bali
sasa nimepatikana,
Nilikuwa kipofu lakini sasa ninaona.
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Kwani alinipenda kwanza.

¹⁸² Amina. Amina. Kuimba katika Roho! Ninapenda hilo, nanyi je? Loo, ninataka kuketi kando ya kilima ambako kuna kichaka kidogo upande *huu* wa mti wa . . . kutoka kwenye chemchemi za Uzima ndipo nisikie zile sauti kuu, sauti zenu zote kuu, Malaika wakiungana pamoja nanyi kule wakiimba upande wa pili wa Mto, ninataka kuketi na kusikiliza kwa miaka elfu kumi. Loo, naam. Loo, jinsi ninavyompenda! Yeye si ni wa ajabu? Bila shaka.

¹⁸³ Sasa, unajisikia vizuri sana? Sasa huko ndiko ninakoita uimbaji wa mtindo wa kale, kuimba katika Roho. Afadhali niwe nako kuliko nyimbo hizi zote ndogondogo, zilizokatwakatwa mnazoimba. Nafikiri hao waandishi waliovuviwa, walipoandika hizo nyimbo. . . Kama vile Eddie Perronet alivyoandika ule wimbo wa uzinduzi wakati alipochukua kalamu yake. Kila mtu alikuwa, hangenunua mashairi yake na kadhalika, basi siku moja Roho akamshukia, akanyakua kalamu, akaandika ule wimbo wa uzinduzi:

Wote wahimidi nguvu za Jina la Yesu!
Malaika na wasujudu;
Leteni taji ya kifalme,

Na kumtawaza kuwa Bwana wa wote.

Mwingine aliandika:

Ninapochunguza msalaba wa ajabu,
Ambapo Mfalme wa Utukufu alifia
Sifa zangu zote ni hasara tu.

Mwingine aliandika:

Alipoishi, Yeye alinipenda; akifa, Yeye
aliniokoa;
Alipozikwa, alizipeleka dhambi zangu mbali
sana;
Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele:
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku yenye utukufu.

Ninawazia juu ya kipofu Fanny Crosby. Kasema, “Yesu anamaanisha nini kwa . . .?” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . unapozuru wengine,
Usinipite.

Wewe ndiwe Kijito cha faraja yangu yote,
Zaidi ya maisha kwangu,
Nina nani duniani ila Wewe,
Au nani Mbinguni ila Wewe?

¹⁸⁴ Jamani, jamani, jinsi Yeye alivyo wa ajabu! Sasa, yule Kristo mkuu, wa ajabu, Yule tunayemwambia nyimbo za kale za imani, babu zetu, huko nyuma katika siku za Spurgeon, John Wesley, na Charles Wesley. . . Mimi na Ndugu Moore tulisimama kaburini si muda mrefu uliopita, nililia tu.

¹⁸⁵ Nikawaza, “Ee Mungu!” niliposimama karibu na kaburi la William Cowper pale. Wakati yeye. . . Walidhani alikuwa mwendawazimu. Mtu yeyote aliye wa kiroho anahesabiwa kuwa mwendawazimu, tunajua hilo, mtu yeyote. Kwa hiyo, akaingia katika Roho, akaandika ule wimbo maarufu:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishiya ya Imanueli,
Wakati wenye dhambi wanapotumbukizwa
chini ya hiyo gharika,
Anapoteza waa lake lote la hatia.

¹⁸⁶ Mnajua kilichotukia? Mara baada ya Roho kumwacha, alijaribu kujiua, kujizamisha mtoni. Naam. Roho alikuwa amemwacha, karibu hakujua mahali alipokuwa. Hao watu mashuhuri, walieleweka vibaya!

¹⁸⁷ Nilisimama pale, nami nikawazia: “Wakati Charles Wesley alipokuwa huko chini mtoni siku hiyo, ama kando ya ziwa kwenye kibanda chake kidogo, dhoruba ikatokea, naye alikuwa akijaribu kurudi, shomoro mdogo akaruka kifuani mwake, naye akamshikilia mpaka dhoruba ilipokwishwa, akatoka akamshika kidoleni mwake, naye alikuwa . . . uvuvio ukaja.”

Mwamba wenye Imara, uliopasuliwa kwa ajili
yangu,
Jalia nijifiche Kwako;
Wakati maji yaliyo karibu yakibubujika,
Wakati tufani ingali ni kali,
Nifiche, Ee Mwokozi wangu, nifiche,
Mpaka dhoruba za maisha zitakapopita
Niongoze salama kifuani Mwako.

Loo, jamani, watu mashuhuri!

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha
Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Kwa kutengana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;
Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
Huku akisafiri kwenye barabara adhimu ya
maisha,
Ndugu mpweke na aliyeharibikiwa na meli,
Katika kuona, atatiwa moyo tena. (Ninapenda
hilo.)

Usiniambie, kwa nyimbo za maombolezo,
Kwamba maisha ni ndoto tupu tu!
Nafsi inayolala imekufa,
Na mambo sivyo yanavyoonekana.
Naam, maisha ni halisi! Na maisha ni bidii!
Wala kaburi silo kikomo chake;
Kwa kuwa u mavumbi wewe, mavumbini
utarudi,
Haikusemwa juu ya nafsi. (Loo, napenda hilo!)
Na tuamke tuingie kazini,
Tujitie moyo katika mzozo wowote.
Msiwe kama wanyama bubu, wanaosukumwa!
(Usisukumwe ndani yake.)
Kuwa shujaa katika mapambano!

¹⁸⁸ Loo, jamani, hao washairi na kadhalika hakika
huichangamsha nafsi yangu ninaposoma juu ya hao watu
wacha Mungu walioyaandika, kama ile *Zaburi Ya Maisha*
pale, Longfellow. Na jinsi ambavyo, nafikiri kwamba Mungu
aliandika mambo hayo, hao watu wa kale, kama ilivyosemwa
katika Biblia, wakiongozwa na Roho Mtakatifu waliandika
nyimbo hizo za kale za Damu, *Ninaona Kijito Cha Damu*
Nyekundu, nyimbo hizo zote maarufu, za kale za kanisa,
ni bora zaidi kuliko baadhi ya maskini upuuzi huu mdogo,
uliokatwakatwa tulio nao siku hizi, ndugu, nawaambia ni
zuri zaidi. Ninaupenda huo *Dini ya Zamani Za Kale*, napenda
nyimbo hizo zote nzuri za imani.

¹⁸⁹ Vema. Wakati Roho Mtakatifu akiwa hapa, tutafanyiza mstari wa maombi, na kuwaombea wagonjwa. Kila mtu chukua imani yako sasa, na moyoni mwako, haikulazimu kulisema kinywani mwako, kumbuka, mawazo ya—yako yana sauti kubwa zaidi Mbinguni kuliko sauti yako ilivyo duniani, unaona, sema hivi: “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!” Angalia kama atafanya jambo lile lile alilofanya.

¹⁹⁰ Zakayo, ondoa tu jani lako la mtini wakati mmoja, uchungulie chini, uone kama Yeye si yeye yule jana, leo, na hata milele bado, uone kama hafanyi jambo lile lile. Yeye atakuvuta utoke, aseme nawe, na jambo jema ni: Ataenda nyumbani pamoja nanyi usiku wa leo, mzungumze Naye kabla hamjaenda kulala, wewe na mkeo. Nyumba itabadilishwa, haitakuwa kama ilivyokuwa wakati huo, atakapoenda nyumbani pamoja nanyi.

¹⁹¹ Billy, uko wapi? Gene, Leo, ni nani aliyesambaza kadi za maombi? Wewe? Loo, loo, Billy? Billy yuko wapi? Ati nini? D? Moja hadi mia moja? Kadi za maombi D zilisambazwa leo. Sasa, ili kwamba tusiweze kuchanganyikiwa... Je, tuna nafasi ya kutosha hapo? Nadhani tungeweza kuwasimamisha wachache hapo, wa ndugu zetu.

Ni nani aliye na D, namba moja? Vema, mama, nenda moja kwa moja hapa. Sasa, itikia wito wako. Namba mbili... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹² ...kufanyika, vizuri. Kulikuwako na mtu na mkewe, mara ya kwanza waliyopata kuhudhuria mikutano yangu, walikuwa wameketi kwenye kusanyiko, mama mmoja akaingia, akaketi kando yao, ndipo likamchukiza maskini huyo mama. Mama huyo alikuwa ameketi hapo karibu, maana alikuwa njiani mwake, akamfanya arudi nyuma. Baada ya kitambo kidogo huyo mama akamfanya kusonga nyuma. Yeye ali-... Mwanamke huyu ambaye ilimbidi kusonga nyuma, alimchukia huyo mwanamke aliyemchukia, kwa hiyo akaanza kuomba, akasema, “Bwana, haikunipasa kufanya hivyo. Nisamehe, sikukusudia hilo.”

Ndipo basi, yule mama aliyekuwa mbele aliyekuwa amemchukia, akasema, “Dada, samahani. Sikukusudia kufanya hivyo.”

¹⁹³ Na hao wawili, mume na mke walikuwa wagonjwa. Na, loo, muda mfupi tu baada ya jambo hilo kufanywa, nilimwona Malaika wa Bwana amesimama juu yao, akawaita kwa jina na kuwaponya wote wawili, na kuwarudisha nyumbani kwao. Lake Charles itajua habari zake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹⁴ ...chukua kiti cha nyuma, dada, ndugu. Pendeleaneni. Vema. Ishirini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano. Vema. Ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹⁵ ...Roho akashuka, akamwambia yale aliyofanya siku nzima, na yale aliyokuwa akifanya, kile alichotaka, na loo,

jamani, akasema, “Hakuna haja kwangu kusimama, tena.” Naye huyo akatoka mlangoni. Loo!

Kamwe sitamwacha,
Kamwe sitaacha . . . (Unalimaanisha kweli?)
Kamwe sitamwacha,
Kwani alinipenda kwanza.

Huko chini msalabani ambapo Mwokozi wangu alifia,
Chini . . . kwa ajili ya kutakaswa na dhambi nililia;

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu . . . (Arobaini hadi hamsini sasa.
Arobaini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano.)

Utukufu kwa Jina Lake la thamani!

. . . Damu ilipakwa moyoni mwangu,
Utukufu kwa Jina lake! (Arobaini na sita,
arobaini na saba.) [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . kuokolewa na dhambi kwa njia ya ajabu,
Yesu kwa utamu sana . . .

Pale msalabani ambapo aliniingiza;
Utukufu kwa Jina Lake!

Tunaimba, utukufu kwa ninii Yake . . .

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa tunapoimba.

Utukufu kwa Jina Lake la thamani!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Sasa kwa utulivu. Sasa ingieni katika Roho.

Loo, hapo moyoni mwangu ninii . . .

Je, kadi zote za maombi ziko tayari? Ukiwa na kadi ya maombi, nenda mstarini. Sasa kwa utulivu na kwa uchaji sasa.

Loo, njoni, kwenye Chemchemi hii tajiri na tamu;

Sasa, tupa . . . nafsi yako miguuni pa Mwokozi;
Jitumbukize ndani leo, na ufanywe mkamilifu;
Tunaimba, utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake la thamani!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

¹⁹⁶ Bwana wa thamani, wakati kinanda kinapopiga huo wimbo mzuri wa kale, kuna wengi hapa ndani, Bwana, wanaoweza kushiriki katika ushirika huu, kujua ya kwamba hapo ndipo dhambi zetu zote zilienda, tulipotumbukizwa kwa imani chini ya kile Kijito chekundu, umeme ukimulika, ngurumo zikinguruma,

Damu ya Mwana wa Mungu, mishipa ya Imanueli ilikuwa ikitokwa damu, wakati mvua hiyo ilipomwagika msalabani, imechanganyika na Damu na maji, ikamwagwa juu ya nafsi zetu, Bwana, kwa imani. Daima tutaimba *Utukufu Kwa Jina Lake*. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, Baba.

¹⁹⁷ Sasa, kama vile labda nimeninii tu... Nisamehe tu njia zangu fidhuli, Bwana, za kuleta Neno Lako, bali mimi, ndivyo bora zaidi niwezavyo kufanya. Nami naomba ya kwamba utalipokea, na kupanda ndani ya mioyo ya watu kusudi lake, Baba, ni kuwaletea watu imani.

¹⁹⁸ Sasa, wanajua kile Wewe ulikuwa, kila usiku tumeyaendea Maandiko tofauti mahali fulani kuthibitisha ya kwamba Wewe... ishara zile zile za Masihi, kila mahali katika Maandiko, Yamejaa tu hizo, Bwana. Labda hawakuwa wamelisoma hapo awali, walilipitia moja kwa moja.

¹⁹⁹ Vivyo hivyo na Mafarisayo na Masadukayo wa siku zao, wale walimu, walilipitia moja kwa moja, kwamba Yeye atakuwa hivyo. Hapana shaka siku ile ile aliyosulubiwa, huenda waliimba hekaluni asubuhi hiyo Zaburi 22, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Ee Mungu, fungua macho ya kiroho. Tupe ufahamu, tunapojikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁰⁰ Sasa, hebu kidogo. Sasa, mnaona mstari huo mrefu wa watu. Hakuna njia kwangu kuwa na... Kuna mtu yeyote hapa ambaye hajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano wakati upambanuzi unaninii... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁰¹ ...na—na kama tu nifanyavyo, yeye hula kama mimi, yeye hulala kama nilalavyo, yeye ni—yeye ni mtu ambaye Yesu alimfia.

²⁰² Sasa, ninalaani fundisho la kanisa Katoliki, hiyo ni kweli, bali si Mkatoliki. Bila shaka. Na kama kamwe nikifikia mahali ambapo siwezi kunyosha mkono wangu kwa Mkatoliki kama nifanyavyo kwa Mpentekoste, basi yanipasa nirudi Kalvari tena, nina kasoro; Yesu alikuja kumfikia mtu yeyote. Na kwa Umoja, Uwili, Utatu, Utano, chochote kile, hakuna tofauti, ninataka kuwanyoshea mkono.

²⁰³ Nilipofikia jambo hili kwa mara ya kwanza kama mhudumu wa Kibaptisti, mbona, kundi moja lilisema, “Njoo, ujiunge na kundi letu.”

Hilo lingine likasema, “Njoo ujiunge na kundi letu.”

Nikasema, “Ndugu, nawapenda nyote wawili.”

“Itakubidi kuungana na moja, kamwe hatutaruhusu hilo.”

Nikasema, “Loo, lakini Mungu ataliruhusu, mnaona. Nitasimama moja kwa moja katikati yenu huku nimenyosha mkono pande zote mbili, na kusema, ‘Sisi ni ndugu!’”

204 “Upendo unaokomboa umekuwa ndio wimbo wangu, na utakuwa hata nitakapokufa.” Mnaona? Hiyo ni kweli. Kuwa na upendo moyoni mwako, na uwe mkweli na mwaminifu, na uwe na nia nzuri, na kusudi jema, na Mungu atashughulikia hayo mengine kama nia yako ni sahihi, na lengo lako ni sahihi. Kama lengo lako ni sahihi, na nia yako ni mbaya, haitafaulu. Lakini unapofanya ninii yako. . . Kama unajua ni mapenzi ya Mungu, halafu nia yako ni sahihi, na lengo lako ni sahihi. . .

205 Kama vile sasa, hili hapa kundi la watu. Nimekuwa nikizungumza kuhusu Yeye kuwa ni Masihi ambaye ungali unaweza kumgusa, sizungumzi juu yake kwa sababu *mimi* nafikiri hivyo, ninazungumza juu yake maana *Biblia* ilisema hivyo. Sasa, sababu. . .

Unasema, “Ndugu Branham, hivi huogopi Yeye ataninii. . .?”

“La, bwana.”

206 Sasa, kama nilitaka kusema, “Angalia hapa, ninaweza kufanya *hivi*. Mnaona jinsi nilivyo mtu mkubwa?” Afadhali ninyamaze, na kuondoka jukwaani papo hapo, maana kamwe haitafaulu. Mnaona?

207 Nia yangu ni nini? Kuwayeyusha watu hawa pamoja, kama watu wa Mungu.

208 Wasema, “Nawaambia, ninyi watu wote, mimi ni wa Baptisti, nyote njoni huku, mkajiunge na Baptisti.” “Mimi ni wa Umoja.” “Mimi ni wa Utatu.” “Mimi ni wa Utatu,” ama “Uwili,” ama chochote ulicho nacho, sijui. Wote: “Mimi ni mfuasi wa *hilo*.”

209 La, bwana. Mimi ni ndugu yenu, mimi ni wa Kristo, sisi ni viungo vya mwili mmoja. Kwa hiyo hilo linafanya nia yangu, kusudi langu kuwa sahihi, nia yangu ni sahihi, kwa hiyo basi, Yeye alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usiwe na shaka.” Na ni mapenzi ya Mungu kwangu kufanya hivyo, la sivyo Yeye kamwe asingenituma, haya basi. Kama ukifanya kila kitu vizuri, na nia yako na kusudi lako ni sawa, unaweza kuambia chochote, maadamu ni mapenzi ya Mungu, kitatendeka.

210 Lakini kama ninataka, tuseme, kuwa mwenye kiburi sana, kujifanyia mpango mkubwa sana mahali fulani, na kujiweka kwenye televisheni, kote ulimwengumi, ama chochote kile, sasa hilo ni kosa. Sininii. . .

211 Yesu alipungukiwa na kitu kimoja. Mnajua kilikuwa kipi? Maonyesho, Yeye hakuwa mtu wa maonyesho. Mnaona? La, la, la. Wao walisema, “Kwa nini unajipumbaza na kundi hili la watakatifu wanaojibingirisha hapa chini, wavuvi, na kadhalika?”

Ndugu yake akasema, “Njoo huku kwa kuhani mkuu. Njoo huku, na ujionyeshe, yale unayoweza kufanya, kama wewe ni *Nanii*.”

Akasema, “Wakati wenu upo sikuzote, Wangu haujafika bado.”

²¹² Hiyo ni kweli. Hakuenda nao, hata pamoja nao, haendi nao siku hizi. Yeye si mtu wa maonyesho, Yeye ni Mwana wa Mungu. Amina. Tunaamini hilo. Loo, Yeye si ni wa ajabu? Yesu, Mwana wa Mungu.

²¹³ Sasa, siwezi kuwa na upambanuzi katika mstari huu, mnaona, bali tutaomba. Kabla sijafanya hivyo, ninataka kuwa na hakika, nikiweza, Roho Mtakatifu atanisaidia, kujua ya kwamba nguvu za Mungu ziko hapa, kwa hiyo unaweza kuona upako.

²¹⁴ Sasa angalieni, kusanyiko hili lote, hebu tufanye tu hili shindano la kuamua usiku wa leo, mnaona, kusanyiko hili hapa nje, kila mmoja ni mgeni kwangu. Kuna mtu mmoja tu... Wasichana hawa wawili wadogo walioketi hapa, hao ni wasichana wa rafiki yangu, maskini wasichana wa Evans. Ndugu Evans, uko wapi? Sijakuona.

Nitawaambia jambo fulani juu ya Ndugu Evans, tunapongojea. Ninangojea kitu fulani. Tulikuwa tukivua samaki si muda mrefu uliopita.

²¹⁵ Jinsi nilivyopata kufahamiana na mtu huyu mzuri na mkewe, Ndugu Mercier alinitambulisha kwake. Asubuhi kabla sijaondoka hotelini (Hivi hiyo haikuwa ni huko Philadelphia pamoja na Theo Jones huko Met?), naye Ndugu Mercier akasema, “Kuna mtu mzuri jina lake Welch Evans, anataka kukutana nawe,” mke wangu alikuwa pamoja nami. Niliamka asubuhi hiyo, pamoja na mvulana wangu mdogo, Joseph. . .

²¹⁶ Nyote mnajua kuhusu mtoto Joseph, miaka sita kabla hajaja, nilimwona katika ono. Daktari alisema mke wangu asingeweza kupata mtoto mwingine, nikasema, “Loo, naam!”

Kwa hiyo wakati mtoto wa pili alipozaliwa, alikuwa ni msichana. Wakasema, “Uh-huh. Ulimaanisha *Josephine*.”

²¹⁷ Nikasema, “Nilimaanisha *Joseph*!” Mungu kamwe hasemi uongo.

²¹⁸ Na sasa, kwa hiyo yapata miaka minne baadaye, yeye, tulijua alikuwa na mimba tena, kwa hiyo wakasema, “Huyu ni Joseph?”

Nikasema, “Sijui.”

Daktari akasema, “Hawezi kumzaa, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Atamzaa huyo.”

²¹⁹ Kwa hiyo, wakati nesi aliposhuka, nilikuwa nikitembea kwenye zulia sakafuni, mwajua. Ndipo akashuka, na kusema, “Kasisi Branham?”

Nikasema, “Naam, mama?”

Kasema, “Una mvulana mzuri, ratili saba na wakia tatu.”

Nikasema, “Joseph, umechukua muda mrefu sana kuja. Baba ana furaha kukuona!”

Na kwa hiyo, akasema, “Ulimwita *Joseph*.”

Nikasema, “Hilo ndilo jina lake.”

²²⁰ Naye Joseph alikuwa pamoja nami kule, akiwa na umri wa miaka minne, imekuwa miaka miwili iliyopita, la, alikuwa na umri wa miaka mitatu, na, yeye ana miaka mitano sasa, naye anaona maono, na alipoamka asubuhi hiyo, alisema, akiketi kando ya kitanda, mimi na yeye hulala pamoja tumekumbatiana, nasi ni marafiki sana, naye akasema, “Baba,” akasema, “David ataumia juu ya pikipiki. Atachuna ngozi ya mguu wake upande ule.”

Nikasema, “Je, uliota hilo?”

Akasema, “La. Baba, nililiona papo hapo.”

²²¹ Tuliliandika tu kwenye kitabu. Tulipofika nyumbani, David, yule mvulana mdogo jirani yetu, siku mbili baada ya sisi kuwa nyumbani, aliendesha pikipiki uchochoroni na kuchuna ngozi ubavuni mwake, kama tu vile alivyosema.

²²² Nitaondoka moja ya siku hizi, enyi marafiki, nitaondoka ulimwenguni. Ninaomba ya kwamba Mungu ataichukua roho ile ambayo amenijalia kuwa nayo, na kuweka sehemu maradufu juu ya mwanangu, Joseph, apate kuangaza Nuru wakati nimeondoka.

²²³ Na kwa hiyo basi, nilimtarajia Billy... Billy ni mmoja wa wavulana wazuri sana ulimwengu ungeweza... Hakuitwa katika huduma. Sasa, sitaki kuondoka bila ya kuwa na mtu wa kuwakilisha, kuchukua mahali pangu wakati nimeondoka.

²²⁴ Basi nikaanza kusogea, ndipo nikamwona Ndugu Welch Evans (Sipaswi kusema jambo hili, Dada Evans. Utanisamehe?), alikuwa amevua samaki wengi kupita kiasi, naye alikuwa akiwaficha kutoka kwa mlinzi wa wanyama pori. Nami nikamwona huko juu katika ono, walikuwa wamewaweka kwenye gunia, naye akawaficha mara mbili ama tatu. Ndipo nikasema, “Sijui kama huyo ni mtu yule yule? Wananiambia anapenda kuvua samaki huko chini Florida.”

²²⁵ Kwa hiyo nikaenda kule asubuhi hiyo. Nilipoingia, mimi na Ndugu Mercier kule nyuma, tuliingia pamoja, nami nikasema, “Huyo ndiye yule mtu. Huyo ndiye.”

²²⁶ Kwa hiyo baada ya kunitambulisha kwake, nikasema, “Bw. Evans?” nami nikazungumza naye. Nikasema, baada ya sisi kuzungumza kidogo, nikajitayarisha kuondoka, nikasema, “Ndugu Evans, unanipenda?”

Akasema, “Hakika.”

²²⁷ Nikasema, “Hapa si muda mrefu uliopita ulikuwa ukivua samaki katika aina fulani ya mbuga ya kinamisi. Ulikuwa na

gunia lililojaa samaki, ulikuwa ukijaribu kuwaficha kutoka kwa mlinzi wa wanyama pori.”

Akasema, “Loo, jamani, jamani!”

Nikasema, “Nitakuomba jambo moja tu: Nipeleke nikavue samaki huko.”

Akasema, “Vema.”

²²⁸ Kwa hiyo ndugu yake ni mwenye dhambi, naye aliumwa na nyoka mchacharisha wa ardhini. Kuna mtu anayejua mchacharisha wa ardhini ni nani? Yeye ni mbaya kabisa. Basi ndugu yake alikuwa hospitalini, naye akatembea kwa mkongojo mduara kwa muda mrefu, sivyo, Ndugu Welch? Kwa mkongojo mduara.

²²⁹ Kwa hiyo, mimi na Ndugu Welch tulirudi kule, tukakamata samaki wakubwa kumi na mmoja siku hiyo. Loo, jamani, ni wazuri jinsi gani! Nami nilikuwa nimemshika samaki mkubwa mno, nisingeweza kumshikilia. Ndipo Ndugu Welch akaja pale, alikuwa amekunja miguu ya suruali yake, akasema, “Kwani huwezi kumshika?”

²³⁰ Nikasema, “Yeye ni mkubwa mno! Hapana shaka ana uzito wa ratili kumi na nne, kumi na tano.” Nami nilikuwa nimemshikilia pale, naye akapitia tu juu ya hizo pedi, nami nikarusha hicho chambo kidogo nje tena, huyu hapa anakuja. Ndipo mmoja akaimeza tena, naye alikuwa mzuri, karibu ratili nane ama kumi, bali nisingeweza kumshikilia. Basi baada ya kitambo kidogo nikamshinda, nikaanza kumvuta ndani.

²³¹ Ndugu Welch akasema, “Nitamkamata.” Na bila ya kuwazia, akaruka ndani ya manyasi hayo na chini ya hizo pedi, ili kumshika huyo samaki miguu mitupu, ndipo mchacharisha wa ardhini akamwuma. Nyoka huyo akapitia kwenye. . .

²³² Naye akaruka akatoka pale, alikuwa ameushikilia mguu wake namna *hiyo*, kana kwamba mfupa unaganda mle ndani, na meno yake yakashikana, machozi yakitiririka mashavuni mwake.

²³³ Nami nikaangalia, damu ikitoka mahali pawili, karibu upana *huo*, kasema, “Loo, jamani!” Vema, mimi. . . Yeye ni mtu mkubwa mno. Nitambebaje yapata maili mbili ama tatu kupitia kwenye vinamasi? Ndipo nikawaza. Nami nikasema, “Loo, Ndugu Evans! Loo, jamani, Ndugu Evans!”

Ndipo Kitu fulani kikaniambia, “Mimi ni Msaada upatikanao sana wakati wa shida.” Sijawahi kuliona hapo kabla.

Nikaweka mikono yangu juu ya mguu wake, kisha nikasema, “Sasa, Ndugu Evans, hebu—hebu kidogo.”

²³⁴ Nami nikasema, “Baba wa Mbinguni, tuko katika hali ya hatari. Nami na—najua ya kwamba Neno Lako linasema,

kwamba watavikanyaga vichwa vya nge na nyoka, wala hakuna kitu kitakachowadhuru. Mtu huyu ni mwaminio, Yeye ni mtoto Wako. Nami ninaweka mkono wangu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, ninaikemea hiyo sumu ya nyoka!”

Ndipo nikamsikia akiacha kuguna, nikaondoa mkono wangu, akasema, “Sina maumivu.”

235 Tuliendelea kuvua samaki siku hiyo yote. Usiku huo walipoingia, walikuwa karibu pale wakizungumza, tulikuwa na hao samakibu wakubwa mno weusi, yapata urefu *huo*, wakining’inia.

236 Yapata saa tano ndugu yake akaja pale, kwa hiyo alikuwa angali anachechemea kidogo kwa mguu wake. Wala hakuwa mwaminio, alikuwa ni mvulana mwenye dhambi, jamaa mzuri, mtu mzuri sana. Ninatarajia kumwongoza kwa Kristo wakati mwingine nitakaposhuka kwenda kule, nimbatize huko nje, moja ya vidimbwi hivyo.

237 Na kwa hiyo, ndipo tulipoenda huko nje, basi ana duka la chambo, nasi tulikuwa mahali fulani katika hoteli ndogo ng’ambo ya pili ya barabara kutoka kwake huko Fort—Fort Pierce. Na kwa hiyo, ndugu yake akaja pale, nami nilikuwa nikimwambia ndugu yake kuhusu jambo hilo. Naye akaona huo mwumo wa nyoka, akasema, “Sasa, Ndugu, ni vema kuwa wa kidini, bali si mwendawazimu!” Akasema, “Afadhali umwone daktari sasa hivi!” Kasema, “Unajua jinsi hiyo ilinifanya nilale hospitalini namna hiyo.”

238 Ndugu Evans akasema, “Niliumwa asubuhi ya leo saa tano, hii ni karibu saa tano usiku wa leo, na Mungu amenilinda kwa neema Yake muda huu, Yeye atanilinda hadi mwisho.”

239 Kamwe hokusuguliwa wala kunusa chochote. Ni neema ya ajabu, Bwana wetu Yesu Kristo.

240 Ninawajua hao wasichana wadogo, Ndugu na Dada Evans. Nami ninaamini huyu ni Ndugu Willie aliyeketi hapa, yule msanii aliyechora picha zao... ulimwengu wa kanisa. Hivi ulikuwa...? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... hiyo Nguzo ya Moto. Ulikuwa huko, Willie, kuona jambo hilo? Ulikuwapo, Ndugu Evans? Dada? Ni wangapi walioko humu jengoni waliokuwa kanisani asubuhi hiyo, kuiona? Vema. Kwa dakika kumi na tano ilisimama pale pale, ikionekana mbele ya karibu watu mia nne wamesimama pale wakiiangalia. Amina. Hiyo ni kweli. Yeye ni Bwana Yesu, na Malaika yuyo huyo wa Mungu yuko papa hapa sasa. Mwaminini Mungu.

241 Sasa, kwenu mlio huko nje, tunaweza kuupitisha mstari huo katika yapata dakika kumi, tunaweza tu kumfanya Roho Mtakatifu atembe pamoja nasi. Bwana anajua ninashuhudia ili kwamba tu mtaona kuijenga imani yenu.

²⁴² Kama ningeanza kusimulia yale nimemwona akifanya, kufanya katika hii, huduma yangu, ambayo nimemwona Yesu Kristo akifanya mbele ya macho yangu, wangeandika vitabu vingi. Kila siku tu, kila saa, unaweza tu kumwuliza Ndugu Moore, watu hawa wanaozunguka, mahali popote, mahali popote, ni kila mara wakati wote, nyumbani, huko nje, na popote pale, Roho Mtakatifu akionyesha tu, ananiondoa mahali, anipeleke *hapa, hapa*. Kama ukijitolea tu Kwake, unaona? Hiyo ni kweli.

²⁴³ Enyi ndugu mnaojua, ambao mmekuwa mikutanoni, na mnajua, ama mmekuwa pamoja nami mikutanoni, na juu—juu nyumbani, na kila mahali pengine, mambo hayo ni kweli, ndugu? Inueni mikono yenu kama ndivyo yalivyo. Hiyo ni kweli. Maelfu wanaweza kushuhudia jambo hilo.

²⁴⁴ Sasa iweni na imani. Na kama Roho Mtakatifu atatuonyesha...Ni nini...? Wawili au watatu ni shahidi. Hiyo ni kweli? Wawili au watatu ni shahidi. Iweni na imani sasa. Inueni mikono yenu tena sasa, ili niweze kuona.

²⁴⁵ Hakuna kadi za maombi. Kama una kadi ya maombi, ingia mstarini. Ni, wewe ni mgonjwa, nami sikujui, ama una haja moyoni mwako, ama chochote kile, inua mikono yako juu. Wengi mno.

²⁴⁶ Una moja? Wewe? Hebu mimi na wewe tuzungumze, wewe uko karibu sana nami. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaniamini mimi? Kama ninaweza, kwa Roho Mtakatifu, kukufunulia shida yako ni nini, utaikubali kama kutoka kwa Bwana?

Je, wasikilizaji wengine watafanya jambo lile lile?

²⁴⁷ Mungu, ni kwa ajili ya utukufu Wako.

²⁴⁸ Una shida ya magoti na miguu yako. Hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Vema, nenda nyumbani ukapokee uponyaji wako, Yesu Kristo anakuponya.

Kuna mtu mwingine unayeamini kwa moyo wako wote? Ngojeni, Hii hapa inaenda, Hii hapa, ngojeni kidogo tu.

²⁴⁹ Mtu huyo aliyeketi papo hapo, akimwombea mama yake hospitalini, ugonjwa wa moyo. Unaamini ataponywa, Ndugu? Vema, bwana. Mungu akubariki.

²⁵⁰ Mimi ni mgeni kwa mtu huyo. Simjui. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, hata hivyo, sivyo? Unaamini sasa? Wa—wanagusa nini?

²⁵¹ Huyu hapa maskini mama mmoja ameketi hapa akiomba kwa moyo wake wote, si kwa ajili yake mwenyewe, kwa ajili ya wokovu wa mumewe. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako, mama.

Vema. Laiti ungalimwamini Mungu!

²⁵² Huyo hapo huko nyuma, ugonjwa wa ngiri, ugonjwa wa moyo. Loo, jamani, ni kila mahali tu. Mnaamini sasa? Ni wangapi wanaoamini kwa mioyo yenu yote sasa? Inua tu mkono wako. Hiyo inaenda tu kuninii... Siwezi kuingia katika hiyo kwa kilindi sana, kwa sababu nisingeweza kuumaliza huu mstari.

²⁵³ Yeye ni Mungu huko nje? Yeye ni Mungu hapa juu? Yeye ni Mungu Mbinguni, Yeye ni Mungu duniani, Yeye ni Mungu kila mahali. (Inanibidi kupata tu dakika moja, Ndugu Jack, kufika upande huu. Unaona?) Je, unaamini yale ambayo umesikia na kuona? Unaamini yanatoka kwa Mungu? Je, watu huko nje wanaamini vivyo hivyo?

²⁵⁴ Kama Mungu atamfunulia mwanamke huyu shida yake ni nini, ama, chochote kile, sijui. Hatufahamiani, nadhani, sisi kwa sisi. Wewe ni... Yeye ni... Alikuwa na kadi ya maombi, sivyo? Vema.

²⁵⁵ Kadi ya maombi, huyu mvulana huja tu na kuchanganya kadi hizi za maombi, na ilitokea tu kwamba ulichukua moja, hivyo tu, unaona. Unaona kile anachoweza kufanya huko nje. Sasa, je, hiyo ndiyo ishara ile ile ambayo Yesu alionyesha na kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi alipokuwa hapa duniani? Unaamini hilo? Unaamini.

²⁵⁶ Nawe unaamini ya kwamba Yesu yuko hapa duniani, usiku wa leo, katika umbo la roho, anayeitwa Roho Mtakatifu; naye anaishi katika Kanisa Lake kwa Damu ya Dhabihu Yake; alifungua na kupasua pazia kwa kumwagwa kwa Damu Yake, na kufanya njia ambayo mimi na wewe tungeweza kuingia katika ule Utukufu wa Shekina, ili Yeye aweze kuzungumza hapa, achukue midomo yangu na kusema nanyi kama waaminio wawili, na kutembea kati yetu, na kunena kati yetu, na kunifunulia mambo yale hasa aliyofanya pale kuthibitisha ya kwamba Yeye hajafa, bali yu hai milele?

²⁵⁷ Huko hapa kwa ajili ya uponyaji, umeponywa. Hiyo ni kweli. Lakini uko hapa kwa ajili ya mume wako. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Vema, ana ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli. Una mwana, hiyo ndiyo sababu ungali umesimama umeinua mkono wako. Unataka nikwambie mwanao ana shida gani? Ana shida na bega lake. Hiyo ni kweli kabisa.

²⁵⁸ Ninamwona mvulana mwingine, ni mpwa. Naam, bwana. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake? Vema. Shida ya mpwa wako, ana shida ya tumbo, ana wasiwasi. Na hapa kuna mambo mawili wote wawili wanahitaji, ni wokovu, maana wote wawili ni wenye dhambi. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Amini sasa kwa moyo wako wote.

Baba Mungu, msichana huyu mdogo mpendwa...

Ninyi nyote ombeni pamoja nami, tafadhalini, sasa kwa ajili ya watu hawa.

Baba, ninaomba ya kwamba utamponya mtoto huyo mdogo na kumpa afya, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

Hilo ni sawa.

Mungu, katika Jina la Kristo mponye.

Njoo, Dada.

Kila mtu akiomba sasa.

Sasa, Dada, kama ningeweza kuunyosha mkono wako, ningefanya hivyo, siwezi, bali ninaweza kuomba.

²⁵⁹ Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya, mkono huu na unyoke. Jalia aende kama Bartimayo akiwa amefunguliwa macho, atoke kwenye jukwaa hili akiamini. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki sasa, Dada.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaushika mkono wa mwanamke huyu na kuomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki.

²⁶⁰ Sasa, unajua ninajua shida yako, lakini kama ningelisema au nisiseme, ungeamini, kwa vyovyote vile? Mnaona, kama nikiendelea na upambanuzi wote mkamilifu, mnajua unavyofanya? Unanivuruga. Lakini mgongo wako uliponywa ukiwa umeketi kitini, kwa hiyo nenda zako nyumbani...?...

Na kama utaamini kwa moyo wako wote, yabisi kavu haitakusumbua tena. Nenda, ukiamini...?...

Bwana, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya, katika Jina la Yesu. Amina.

Liamini. Nenda ukiamini...?...

Baba yetu wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada yangu na kuomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu.

Rudini kwenye...?...Endeleeni kuomba. Endeleeni kuomba.

Maombi yenu, marafiki, ninyi ni Kanisa la Mungu. Waombeeni watu hawa. Vipi kama ni mama yako, baba, mume wako, mke?

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya, katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

²⁶¹ Wakati upako wa Roho Mtakatifu unapokuja sasa, wewe njoo tu ukiamini kwa moyo wako wote, na Mungu ata—ataponya. Unaamini hilo? Unaamini?

²⁶² Mimi—mimi...Sikilizeni, enyi marafiki, kama tu nikiwafanya mnyamaze kwa dakika moja tu, sikilizeni. Haijalishi ni wapi...Unaona, hupaswi kuwazia ya kwamba Roho Mtakatifu ameondoka hapa, kwa sababu sizungumzi na

kila mmoja. Ningeninii... Wangekuwa tayari wamenitoa nje, kama ingalikuwa hivyo. Ni wangapi wanaotambua ya kwamba Bwana wetu, wakati yule mwa—mwanamke alipogusa vazi Lake, alihisi nguvu zikimtoka? Vipi...? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ni wangapi wanaojua ya kwamba nabii aliyeitwa Danieli aliona ono moja, naye alifadhaika kichwani mwake siku nyingi kwa ajili yake?

²⁶³ Mnafikiri ninawajuaje watu hao, yote kuwahusu, na mambo kama hayo, kama haikuwa ni ono? Ningewezaje kamwe kujua jambo hilo? Basi mnaona ninalomaanisha? Nguvu... Mimi... Kama nikininii tu... Ninawaona watu wakija. Unahisi mtetemo huo ukiwapiga, halafu inakubidi tu ku—inakubidi tu kugeuza kichwa chako, na kuweka mikono yako juu yao na kuendelea. Sababu ya Roho Mtakatifu kuwa hapa, atafanya kazi ile ile, Bwana atafunua. Si kwa sababu tu huyo alipita, ama kitu fulani.

²⁶⁴ Hapa, anayefuata yuko wapi? Je, huyu...? Hapa. Vema. Hatufahamiani, sivyo? Sikujui, hunijui mimi. Kama hiyo ni kweli... Umenisikia nikihubiri hapo awali, lakini kukujua, labda tu uliketi kwenye kusanyiko mahali fulani. Unaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Kama nitaweza basi, kwa neema ya Mungu, kuwafunulia kwa Roho wa Mungu, mambo...

Unasema, “Kwa nini unazungumza juu yangu, Ndugu? Kwa nini unaninii...?”

²⁶⁵ Ninaishika roho yako, kama tu vile alivyomshika yule mwanamke kisimani. Itakubidi, kuamini neno langu kwa jambo hilo. Lakini kama akitangaza kwamba ni kweli, basi ni kweli, nilisema kweli. Unaona? Halafu basi, kama nikidai kwamba si mimi, kwamba ni Yeye, nimesema kweli. Hilo hapo Neno Lake, linatangaza jambo hilo. Unaona? Ni kwa mapenzi Yake ya kuruhusia ambapo ninafanya hivyo. Mnaona? Ananiruhusu kufanya hivyo.

²⁶⁶ Sasa, unasumbuliwa na wasiwasi, wasiwasi kabisa. Hiyo ni kweli. Nawe umefanyiwa upasuaji, upasuaji kwenye tumbo. Hiyo ni kweli kabisa. Hutoki kwenye mji huu, kutoka mahali panapoitwa Vidor, ama kitu kama hicho. Vidor. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Vema, Bibi Beech, unaweza kurudi nyumbani, uwe mzima...?...

²⁶⁷ Unaamini? Sasa, endeleeni tu kuomba, endeleeni katika maombi wakati watu hawa wakipita, endeleeni tu kuomba.

Bwana Yesu, mponye mtu huyu, ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu awabariki. Nenda zako ukishangilia sasa.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...hii, ninaomba maombi ya imani kwa ajili ya ndugu yangu, katika Jina la Yesu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...sasa, kwa moyo wako wote, usiwe na shaka. Amini kwa moyo wako wote, utakuwa sawa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...mtu, unaonekana kuwa na roho nzuri. Wewe ni Mkristo. Unaamini kwa moyo wako wote Mungu anaweza kuniambia shida ni ipi? Unafikiri mume wako atapata afya, huo ugonjwa wa jicho, kuwa na mzio, na kadhalika? Nenda ukaamini sasa, naye atapona. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...mponye katika Jina la Yesu. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...Lubbock. Mungu akubariki, Dada.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaweza kukumbuka wakati nilipoingia kwenye chumba cha faragha kuomba wakati dha-dharura ilipotokea, na ni jambo kubwa jinsi gani ulilofanya nyumbani mwao. Ninaomba, Baba, sasa nikijua kuna shida gani, Ninaomba ya kwamba Wewe utambariki na kumpa shauku ya moyo wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁶⁸ Unaamini Yeye atakuponya? Naam. Okoa upasuaji huo, akufanye mzima, kama unaamini. Unafikiri ni nini? Vema, mlidhani ilikuwa ni uvimbe, ni kikulia, mlidhani ilikuwa ni uvimbe, mlidhani ilikuwa ni kansa. Ulikuwa na mambo mengi, lakini inaleta tofauti gani, maadamu Yeye anayaponya? Hiyo ni kweli? Unachohitaji ni kuinuliwa kidogo katika imani, sivyo? kukufanya uinuke. Sarah, nenda nyumbani, na uwe mzima. Yesu Kristo anakuponya...?...

Baba Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, mponye. Rehema za Mungu na ziwe pamoja na mtoto huyu. Mpe afya. Mama na aone tofauti kubwa ndani yake, Bwana! [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Yesu, na iwe hivyo... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Katika Jina la Bwana Yesu, dada yangu na aponywe. Amina.

Uliza nayo... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Mpe ujasiri wa kuwa na imani na kuamini. Baraka zako ziko juu yake, zimekuwako tangu kiamshakinywa. Ninaomba ya kwamba utamjalilia kuliona, Bwana, na kujua ya kwamba mishipa hii iliyovutika itarekebishwa. Katika Jina la Yesu. Amina.

Usiwe na shaka, wewe amini.

Njoo, ndugu yangu.

Baba yetu wa Mbinguni, ninapoweka mikono juu yake, katika Jina la Bwana Yesu, naomba, wakati mpendwa wake

akimwongoza, Kristo na aongoze tangu sasa, Bwana mpendwa, akimpa afya, akimrejesha moja kwa moja tena. Amina.

Usiwe na shaka.

Njoo, amini.

²⁶⁹ Unaamini? Kila mtu unaamini kwa moyo wako wote? Iweni tu na imani.

U hali gani? Kijana mwenye nguvu, anayeonekana mwenye afya, lakini huwezi daima kuenda na hilo. Unafikiri Roho Mtakatifu anaweza kuniambia shida yako? Unaamini?

Wasikilizaji wanaamini jambo lilo hilo? Kama Kristo anabaki Kristo, Yeye anaweza.

²⁷⁰ Kitu cha ajabu kwako, hiyo ndiyo sababu Yeye alinisimamisha. Loo! Ninawathamini. Sasa, kuponya, siwezi kuponya, mama, mimi ni mwanadamu. Lakini hayo maisha hayawezi kufichika sasa. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, mgonjwa sana, unaiita kansa katika mkondo wa damu, jina linalofaa ni lukemia. Hospitalini, si hapa, huko Louisiana. Hiyo ni kweli. Hiyo ni imani nzuri kwa mwenye dhambi kuwa nayo. Je, utamkubali Yesu kama Mwokozi wako binafsi sasa? Utamkubali? Vema. Inua mikono yako. Na usamehewe dhambi zako...?...

²⁷¹ Amina. Unaamini? Ni wangapi, hapa, walio tayari kumpokea Kristo kama Mponyaji? Ninawapa changamoto kuamini. Je, imani yako yaweza kumsimamisha? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, kila mmoja wenu, anayetaka uponyaji, simama kwa miguu yako. Sijali una shida gani, simama na ukubali uponyaji wako. Inueni mikono yenu.

²⁷² Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, Mpaji wa kila karama njema, ninampa ibilisi changamoto katika imani safi.

²⁷³ Toka ndani ya watu hawa, Shetani! Umeshindwa vita, katika Jina la Yesu, waache!

²⁷⁴ Inueni mikono yenu sasa, mkamsifu.

Nitamsifu, nitamsifu,

²⁷⁵ Inueni mikono yenu, mkamsifu. "Mpeni utukufu, enyi watu wote." Mnamkubali? Semeni, "Amina." Je, mnamkubali kama Mponyaji wenu? Je, mnamkubali kama Mwokozi wenu? Basi inueni mikono yenu, na kusema, "Mungu asifiwe." Ninawatangaza wazima, katika Jina la Yesu Kristo. 

61-0124 Bartimayo Kipofu
American Legion Hall
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org